Haliuzwi
DESEMBA 2, 2025
/islamicftz
Jumada II 11 1447

# IMAAN

ISSN 5618 - NO. 560

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

## Qatar yaipa Tanzania magari maalum kuhudumia viongozi





# The Islamic Foundation yasaidia Kigoma gari ya wagonjwa




## Wanacho tarajia wananchi Rais Samia akihutubia Taifa

Mtaalamu: Fedha za Kiislamu zilitangulia ESG, Dunia inaiga sasa

## Jaji Othman: Tumejikita kuzingatia Watanzania wanataka nini

## Dkt. Mwinyi: Tuilinde tunu ya amani kwa wivu mkubwa

Masheikh waungana kuhimiza amani khutba za Ijumaa



Mafungamano ya amani na haki katika Uislamu
NA SHEIKH Seif Ruga



Ukatili wa Wabudha kuwalenga Waislamu washtua Dunia

جمادى ثاني

**HABARI MOROGORO**

MRISHO SALUM TOZO




Akipokea gari hilo, Mkurugenzi wa Kigoma wa taasisi ya The Islaamic Foundaation, Senga alitoa shukrani kwa uongozi wa makao makuu wa taasisi hiyo na pia Al Barakah Foundation kwa mchango wao mkubwa katika ustawi wa jamii.

# The Islamic Foundation yasaidia mkoa wa Kigoma gari ya wagonjwa

Taasisi ya The Islamic Foundation imeishi tena katika kauli mbiu yake: 'Tumeahidi, tumetimiza na ALLAH ni shahidi' baada ya kufanikiwa kukabidhi gari ya kubeba wagonjwa mkoa wa Kigoma.

Gari hilo ambalo Mwenyekiti wa taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahdi aliwaahidi wananchi wa mkoa wa Kigoma ilikabidhiowa kwa Mkurugenzi wa TIF Mkoa wa Kigoma, Menshi Omari Senga, Novemba 23, 2025 makao makuu ya taasisi hoyo mjini Morogoro

Mwenyekiti Nahdi alisema ni matarajio yake kuwa gari hilo la kisasa la kubeba wagonjwa litarahisisha upatikanaji wa huduma za afya na kuimarisha mfumo wa dharura mkoani humo.

Hatua hiyo imepokelewa kwa faraja kubwa na viongozi wa sekta ya afya pamoja na wakazi wa Kigoma, ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakikumbana na changamoto ya usafiri wa wagonjwa.

Ikumbukwe kuwa Mwenyekiti wa The Islamic Foundation , Aref Nahdi, alitoa ahadi ya kutoa gari hilo wakati wa ziara yake katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma - Maweni, na kisha kufanya kikao na viongozi wa Jumuiya ya Kuhuisha Tabia za Kiislamu (JAI) mkoani humo.

Katika kikao hicho, viongozi wa JAI waliwasilisha risala yao kwa Mwenyekiti wa taasisi ya The Islamic Foundation kuhusu uhaba wa magari ya kubebea wagonjwa, hali iliyosababisha uchelewaji wa wagonjwa kufikishwa hospitalini, hususan katika maeneo ya vijijini na pembezoni.

Baada ya kusikiliza kwa makini changamoto hizo, Mwenyekiti Nahdi aliahidi kutafuta suluhisho la haraka, akisisitiza umuhimu wa taasisi za dini kushirikiana na Serikali katika kusaidia jamii bila kujali mipaka au kubagua dini za wafaidika.

Katika ahadi yake, Nahdi alisema The Islamic Foundation ingepeleka gari uya kubeba wagonjwa ndani ya muda mfupi. Wiki moja baadaye, ahadi hiyo iligeuka kuwa halisi - shukrani kwa ushirikiano uliotolewa na Al Barakah Foundation katika kufanikisha upatikanaji wa gari hiyo mpya yenye vifaa muhimu vya dharura, ikiwemo mashine ya oksijeni, vitanda maalumu kwa wagonjwa, vifaa vya kupima viashiria muhimu na eneo la kutolea huduma za kwanza.

Msaada huo inshaAllah, utakuwa mkombozi mkubwa kwa huduma za afya mkoani humo na kuokoa maisha —hasa katika wilaya ambazo zimekuwa zikikabiliwa na vifo vinavyotokana na wagonjwa kuchelewa kufikishwa hospitalini.

Katika hafla ya makabidhiano, Nahdi aliwataka viongozi wa taasisi yake wa mkoa huo wa Kigoma kushirikiana kwa karibu na JAI katika kuhakikisha gari hilo linatunzwa na kutumika kwa manufaa ya wote. Aidha, Nahdi aliikumbusha jamii kuwa kaulimbiu ya "Tumeahidi, Tumetimiza na Allah ni Shahidi," si maneno ya kushawishi na kujitapa bali ni mwongozo wa kazi zao za kila siku. Nahdi alisema The Islamic Foundation itaendelea kutekeleza miradi ya kijamii inayolenga kuboresha maisha ya Watanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Akipokea gari hilo, Mkurugenzi wa Kigoma wa taasisi ya The Islaamic Foundaation, Senga alitoa shukrani kwa uongozi wa makao makuu wa taasisi hiyo na pia Al Barakah Foundation kwa mchango wao mkubwa katika ustawi wa jamii. Aliahidi kuwa uongozi wa mkoa utashirikiana na JAI kuhakikisha gari hilo linatumika ipasavyo, linatunzwa, na linatoa huduma bila upendeleo kwa wenye uhitaji.

"Ambulance hii imekuja wakati muafaka. Ni chombo muhimu sana kwa mkoa huu, na tunathibitisha kuwa tutajitahidi kulitunza ili liwe msaada wa muda mrefu kwa wananchi," alisema Senga.

Msaada huo umeelezwa pia kuwa ni kielelezo cha nguvu ya ushirikiano baina ya taasisi za Kiislamu, mathalan katika jambo hili, The Islamic Foundation na Al Barakah Foundation, katika kuhakikisha jamii inapata huduma bora. Ushirikiano huo umeonekana kuwa mfano wa kuigwa kwa taasisi nyingine nchini katika kuchangia maendeleo ya sekta ya afya na sekta nyingine za maendeleo ya jamii na kidini.

NA MWANDISHI WETU

# Matarajio ya wananchi hotuba ya Rais Samia

**Hotuba hiyo itakayotolewa leo, inakuja katikati ya hofu ya usalama waliyonayo baadhi ya wananchi kutokana na maandamano yaliyozaa vurugu ya Oktoba 29 na mengine yanayopangwa kufanyika Desemba 9, kupitia mitandao ya kijamii.**

Macho na masikio ya wananchi yataelekezwa tena Dar es Salaam, ambako Rais Samia Suluhu Hassan anatarajia kulihutubia Taifa kuhusu yanayoendelea nchini, ikiwemo masuala ya usalama na kuliponya Taifa.

Hotuba hiyo itakayotolewa leo, inakuja katikati ya hofu ya usalama waliyonayo baadhi ya wananchi kutokana na maandamano yaliyozaa vurugu ya Oktoba 29 na mengine yanayopangwa kufanyika Desemba 9, kupitia mitandao ya kijamii.



Katika vurugu hizo, baadhi ya watu walipoteza maisha, kujeruhiwa, biashara na mali za watu binafsi ziliharibiwa, kadhalika miundombinu ya umma vikiwemo vituo vya polisi, ofisi za Serikali za mitaa, ofisi za Chama cha Mapinduzi (CCM), Mahakama na vituo vya mafuta vilichomwa moto.

Ni hotuba inayosubiriwa kwa hamu, kwa sababu ndiyo itakayoamua ama kuponya majeraha yaliyomo miongoni mwa Watanzania, au kuja na hatua zitakazojenga mustakabali mwema wa Taifa.

Hotuba hiyo inaibua shauku zaidi hasa ukizingatia inatolewa nyakati ambazo tayari Rais Samia ameshaunda tume kuchunguza kiini cha vurugu na ameshawasamehe vijana kadhaa waliokamatwa kwa kuhusika na matukio hayo.

Novemba 20, mwaka huu, Rais Samia alipoizindua tume hiyo yenye wajumbe wanane ikiongozwa na Jaji Mkuu mstaafu, Othuman Mohamed Chande, aliiagiza kwenda kusaka kiini cha tatizo hilo na kuja na mapendekezo yatakayoweka msingi wa maridhiano.

Rais Samia alisema tume hiyo itafanya kazi kwa miezi mitatu sawa na siku 90: "Mapendekezo yatakayotoka huku (Tume ya Uchunguzi) ndiyo tutakayokwenda kuyafanyia kazi kwenye Tume ya Maridhiano. Kwa hiyo, mapendekezo yenu ndiyo yatafanya ajenda za Tume ya Maridhiano."

Wakati wadau wakisubiri majibu ya tume, jana Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alikutana na waandishi wa habari ofisini kwake na kueleza kuwa kesho Jumanne, Rais Samia atazungumza na wazee wa mkoa huo.

Chalamila alisema kupitia wazee wa Dar es Salaam, Rais Samia atalihutubia Taifa katika ukumbi wa Julius Nyerere kuanzia saa 5 asubuhi. Alisema mkuu huyo wa nchi ataambatana na viongozi wa Serikali na wasio wa Serikali ambao watakuwa na mchango mkubwa kwenye mazungumzo hayo kwa mustakabali wa Taifa. "Ni mkutano mwafaka, unaorejesha matumaini na kuendelea kuponya pale ambapo Watanzania waliumia," alisema Chalamila.

Hata hivyo, baadhi ya wachambuzi waliozungumza na Mwananchi baada ya Chalamila kutoa taarifa yake wamekuwa na mitazamo tofauti hasa ikizingatiwa haikutarajiwa tena kama atazungumza.

Mwanahistoria wa siasa za kimataifa, Dk Azikiwe Boraufe, alisema taifa liko katika "hali tete" inayohitaji hatua za haraka za kurejesha imani. "Kabla Rais hajaongea na wazee, alitakiwa kwanza kukaa na viongozi wake na wasaidizi wake. Lazima tujiulize tumefikaje hapa na tunahitaji nini kutoka hapa tulipo," alisema.

Boraufe alitaja tatizo kubwa la viongozi kupuuza ishara za mgawanyiko katika jamii na taasisi, akitolea mfano mpasuko ndani ya CCM uliowahi kuonekana wakati wa marehemu Bernard Membe na kuibuka upya mwaka huu kupitia mchakato wa kumpitisha mgombea wa urais.

"Hivi vitu tuliviona kama vidogo, lakini sasa vimetuletea majeraha makubwa. Mwangwi wa baadhi ya wanachama kupinga mchakato wa mwanzo wa mwaka huu ulikuwa tahadhari ya wazi," alisema.

Alisema mfululizo wa kukamatwa na kufunguliwa mashtaka kwa wanasiasa umeongeza hasira, huku akisema Rais anapaswa kutumia hotuba hiyo kurejesha matumaini.

"Sasa hatuhitaji kuunganisha vigae vilivyovunjika. Tunahitaji kuchimba udongo mpya na kufinyanga chungu kipya," alisema.

Boraufe pia alipendekeza kufutwa kazi kwa watumishi wote waliohusika na mauaji ya raia wasio na hatia Oktoba 29.

Mwanaharakati wa haki za binadamu, Dk Hellen Kijo Bisimba, alisema hotuba ya Rais Samia ni hatua nzuri, lakini imekuja nje ya wakati.

HABARI ZANZIBAR

NA MWANDISHI WETU



# Dkt. Mwinyi: Tuilinde tunu ya amani kwa wivu mkubwa

Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi amesema kuna umuhimu mkubwa kwa kila mwananchi kutimiza wajibu wake katika kudumisha amani.

Aidha ametoa wito kwa makundi ya wanasiasa, viongozi wa dini na wanahabari kuwa makini na kauli wanazotoa mbele ya jamii kwa kuwa ndiyo makundi yanayosikilizwa na watu wengi na yenye ushawishi mkubwa katika jamii.

Rais Mwinyi ameyasema hayo Ijumaa iliyopita katika msikiti wa Jamiu Zinjibar, Mkoa wa Mjini Magharibi, alipojumuika na Waumini wa Dini ya Kiislamu katika ibada ya sala ya Ijumaa na dua maalum ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuliombea Taifa amani.

Amesema matukio yaliyojitokeza Tanzania bara ni funzo muhimu kwa Watanzania wote, ikiwamo Zanzibar, kwamba hakuna jambo linaloweza kufanikiwa bila kuwapo kwa amani katika nchi. Amefafanua kuwa si suala la maendeleo pekee bali hata ibada haziwezi kufanyika panapokosekana amani.

Amesisitiza wanasiasa, viongozi wa dini na waandishi wa habari kuendelea kuhubiri na kuimarisha amani wakati wote. Pia amewataka viongozi wa dini zote kuwa na kauli zinazohimiza amani kwa wafuasi wao, na kuwataka waandishi wa habari kutumia kalamu zao na mitandao ya kijamii kwa busara na kuacha kuchapisha habari zinazoathiri amani ya nchi.

Amesisitiza kuwa, kila mmoja husuani vijana wanapaswa kulithamini Taifa lao na kuishi maisha yenye nidhamu na hekima kila siku.

# Kongamano La 4 La Afrika Mashariki



Diamond Jubilee

**Disemba 27**

جمادى ثان

HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

# Jaji Othman: Tunajua wanachotaka Watanzania



> Kabla hatujaanza kazi kwanza sisi wenyewe tumejiangalia, wenzetu wanataka nini. Tumebaini watu wanataka uchunguzi kamilifu, usifanyike nusunusu, wanataka uwazi kwenye kazi na kama utachukuliwa ushahidi uwe utakao-tumika sio ambao hauwezi kutumika."
>
> **Jaji Mohamed Chande**

Mwenyekiti wa Tume ya Uchunguzi wa Matukio ya Uvunjifu wa Amani wakati na baada ya uchaguzi mkuu Oktoba 29, 2025, Jaji Mkuu mstaafu, Mohamed Othman Chande amesema anajua utendaji wa tume hiyo utapimwa kitaifa na kimataifa, hivyo imejikita kuzingatia Watanzania wanataka nini.

Miongoni mwa mambo waliyobaini alisema Watanzania wanataka uchunguzi ufanyike kikamilifu, uwazi na ushahidi utakaochukuliwa uwe unaotumika iwapo italazimika kufikia hatua hiyo katika muhimili wa kisheria.

Hiyo ni kauli ya kwanza kwa tume hiyo yenye wajumbe tisa, tangu ilipoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan na kuanza kazi Novemba 20, mwaka huu.

Hata hivyo, kuundwa kwa tume hiyo kuliibua upinzani, baadhi wakiipinga kwa kile walichosema, haitakuwa huru hasa pale itakapolazimika kuichunguza mamlaka iliyoiteuwa kwa kuwa kutakuwa na mgongano wa masilahi.

Baadhi ya wanaopinga tume hiyo wamefungua shauri Mahakama Kuu Masjala Ndogo, Dar es Salaam kupinga uhalali wake kwa hoja kuwa, uteuzi wa wajumbe wake umekiuka haki ya asili.

Shauri hilo la madai mchanganyiko litakalosikilizwa leo lilifunguliwa Novemba 26, 2025 mahakamani hapo na mwanaharakati Rose Mwakitwange na mawakili wa Mahakama Kuu na Mahakama za chini, Edward Heche na Deogratius Mahinyila.

Mahakama hiyo iliwataka mwenyekiti na wajumbe wa tume hiyo kuhudhuria shauri lililowakabili.

Kwa mujibu wa hati ya taarifa, shauri hilo lililosainiwa na kutolewa jana na Naibu Msajili kwenda kwa wajumbe wa tume hiyo, ambao ni wajibu maombi katika shauri hilo, limepangwa kusikilizwa na Jaji Hussein Mtembwa.

"Tambua kuwa kesi tajwa hapo imepangwa kutajwa Desemba 2, 2025, saa 3:00, mbele ya Mheshimiwa H.S. Mtembwa. Unatakiwa kuhudhuria bila kukosa kwa njia ya mtandao na unapaswa kuwasilisha nyaraka zote unazokusudia kuzitumia katika kesi yako," inasomeka taarifa hiyo kwenda kwa wajibu maombi.

Kuundwa kwa tume hiyo, kumetokana na tukio la maandamano yaliyosababisha vurugu wakati na baada ya Oktoba 29, mwaka huu na kusababisha vifo, majeruhi, uharibifu wa biashara, mali za watu binafsi na miundombinu ya umma.

Jana, jijini Dar es Salaam, Jaji Chande alikutana na wahariri na waandishi kwa mara ya kwanza tangu kuzinduliwa kwa tume hiyo.

Alisema ni dhamira yake na wajumbe wa tume hiyo kufanya kazi kikamilifu, kwa viwango kwa kuwa anajua watapimwa kwa utendaji kutoka ndani na nje ya nchi.


"Tunataka tufanye kazi kikamilifu, kwa kiwango kwa sababu tunajua tutapimwa kwa viwango, ndani na nje ya nchi, hiyo tunajua. Tusipimwe kabla hatujaanza mtihani, tufanye mtihani mtupe maksi," alisema.

Kwa sababu hiyo, alisema kabla ya kuanza kazi, wameanza kuangalia Watanzania wanataka nini kutoka kwa tume hiyo ili wayazingatie wakati wa utendaji wao.

Katika mambo waliyobaini wananchi wanataka, amesema ni uchunguzi wa kina usiishie nusu, uwazi na ushahidi utakaochukuliwa uwe ule utakaoweza kutumika katika mamlaka za kisheria.

"Kabla hatujaanza kazi kwanza sisi wenyewe tumejiangalia, wenzetu wanataka nini. Tumebaini watu wanataka uchunguzi kamilifu, usifanyike nusunusu, wanataka uwazi kwenye kazi na kama utachukuliwa ushahidi uwe utakaotumika sio ambao hauwezi kutumika," alisema Jaji Chande. Sambamba na hilo, Jaji Chande alisema wajumbe wote wa tume hiyo wamekula kiapo, hivyo iko huru na wanaanza kufanya kazi bila shinikizo la yeyote na utendaji wao utajikita kwenye hadidu za rejea na ushahidi utakaowaridhisha.

MRISHO SALUM TOZO




# Juhudi za kueneza shule za Imaan nchi nzima zapongezwa

**mpango wa kuanzisha shule zaidi katika mikoa ya Mwanza, Kigoma na Arusha unaonyesha kujitoa kwa taasisi hiyo katika kupanua upatikanaji wa elimu bora nchini.**

TAASISI ya The Islamic Foundation imepongezwa kwa mchango wake mkubwa katika kuboresha sekta ya elimu nchini, hususan kupitia mpango wake wa kufungua shule za msingi za Imaan katika maeneo mbalimbali ya Tanzania.

Pongezi hizo zimetolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya Shule za Imaan, Abeid Mlapakolo, wakati akizungumza katika mahafali ya Shule ya Msingi Imaan yaliyofanyika Kilakala, Manispaa ya Morogoro, chini ya taasisi ya The Islamic Foundation

Akizungumza katika mahafali hayo, Mlapakolo alisema uwekezaji wa The Islamic Foundation katika elimu ni hatua muhimu kwa maendeleo ya taifa. "Hatua ya taasisi ya The Islamic Foundation kuwekeza katika elimu inaonyesha dhamira yao ya dhati ya kuhakikisha watoto wa Kitanzania wanapata elimu bora, yenye maadili na malezi yanayoendana na misingi ya dini na utamaduni wetu," alisema.

Aidha, alibainisha kuwa shule za Imaan zimekuwa mfano wa utoaji wa elimu bora inayochanganya taaluma, maadili, nidhamu na uongozi. "Shule za Imaan zimejipambanua kwa kutoa elimu iliyoandaliwa kwa umakini mkubwa, inayowaandaa wanafunzi kuwa raia wema na chachu ya maendeleo ya taifa."

Mlapakolo alisema mpango wa kuanzisha shule zaidi katika mikoa ya Mwanza, Kigoma na Arusha unaonyesha kujitoa kwa taasisi hiyo katika kupanua upatikanaji wa elimu bora nchini.

"Mpango huu unaonyesha nia thabiti ya mwenyekiti wa taasisi hiyo, Aref Nahdi kujibu mahitaji ya jamii na kuhakikisha kila mtoto anafikiwa na elimu bora."

Kwa upande wake, mgeni rasmi katika mahafali hayo, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Sekondari Forest Hill, Mohammed Muro, aliwahimiza wazazi kuwapeleka watoto wao katika shule hiyo.

"Nawaomba wazazi: pelekeni watoto katika shule za Imaan. Hapa wanapata elimu bora na malezi ya maadili ambayo ni msingi wa mafanikio ya baadaye," alisema Muro. Aliongeza kuwa shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri katika malezi ya dini, hivyo kuzalisha wanafunzi wenye nidhamu, tabia njema na ufaulu mzuri.

Naye Mkuu wa Shule ya Msingi Imaan, Salim Bahanzika, alisema shule hiyo imeendelea kushika nafasi ya juu katika matokeo na nidhamu ya wanafunzi.

Nao baadhi ya wazazi na walezi waliohudhuria mahafali hayo walisema shule hiyo imekuwa chachu ya maendeleo ya jamii ya Morogoro. "Shule ya Imaan ni mkombozi kwa watoto wetu. Mazingira ni mazuri, walimu wana weledi, na nidhamu ni ya kiwango cha juu," alisema mmoja wa wazazi.

جُمادى ثان



# MATUKIO KATIKA PICHA

NA ABDULRAHMAN OMAR

# Juhudi za kueneza shule za Imaan nchi nzima zapongezwa














NA MUGINI SINGIRA



Balozi wa Qatar nchini Tanzania Mh. Fahad al Marekhi akimkabidhi Waziri wa Mambo ya Nje, Balozi Mahmoud Thabit Kombo magari mawili aina ya Land Cruiser Prado

# Qatar yaipa Tanzania magari maalum kuhudumia viongozi wanaozuru nchini

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imepokea magari mawili aina ya Land Cruiser Prado kutoka Taifa la Qatar kwa ajili ya kuhudumia viongozi wanaokuja kwa ziara za kitaifa na kikazi nchini.

Qatar, ambayo ni mshirika muhimu wa maendeleo ya uchumi wa Tanzania, imetoa magari hayo mapya kufuatia ombi la magari na pikipiki za kuhudumia viongozi wa nje wawapo katika ziara nchini huku wakiendelea na mchakato wa kuleta pikipiki sita.

Akizungumza katika ofisi ndogo za Wizara ya Mambo ya Nje jijini Dar es Salaam baada ya kukabidhiwa nyaraka za magari hayo, Waziri wa Mambo ya Nje, Balozi Mahmoud Thabit Kombo ameishukuru Qatar kwa kuwa mdau mkubwa wa maendeleo Tanzania na kuahidi kutumia vyema magari hayo akisema yatatatua changamoto zinazojitokeza katika kazi.

Qatar imekuwa ikishirikiana na Tanzania katika masuala ya ajira na vijana kwa kutoa nafasi za ajira kwa madereva wa Kitanzania nchini Qatar, huku nafasi nyingine zaidi zikitarajiwa kutangazwa.

# Sheikh Mauba: Waislamu shikamaneni, pendaneni

Waislamu wametakiwa kutambua kuwa wao ni ndugu na hivyo kutakiwa kuzidisha mapenzi baina yao, ikiwa ni agizo la Mwenyezi Mungu na mafundisho ya Mtume wake Muhammad (rehema za Allah na amani zimshukie).

Wito huo umetolewa na Sheikh Aman Mussa Mauba wakati akitoa khutba ya sala ya Ijumaa katika msikiti wa Al Wahda Al Islamiya uliopo jijini Mwanza.

"Ndugu Waislamu, khutba yangu nakuombeni tuzidishe mapenzi kati yetu, nakuombenio tufute tofauti zetu, nakuombeni tuache kudharauliana, nakuombeni turudi katika kauli ya Mwenyezi Mungu ' Innamal muuminuuna ikhwa (Waumini ni ndugu)'" Sheikh Mauba alisema. Akikumbusha kuwa Qur'an ndio rejea ya Muislamu,m Sheikh Mauba alinukuu aya kadhaa zinazoagiza kupendana na kutodharauliana.

Katika Sura 49:13, Sheikh Mauba alinukuu Qur'an, ikisema: "Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari."

Katika Qur'an (49:11), Allah anasema: " Enyi mlioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao. Huenda hao wakawa bora kuliko wao. Wala msivunjiane hishima, wala msiitane kwa majina ya kejeli. Ni uovu kutumia jina baya baada ya kwisha amini. Na wasio tubu, hao ndio wenye kudhulumu."

Sheikh Mauba aliwakumbusha Waislamu neema ya Mwenyezi Mungu kwao kwani huko nyuma walikuwa maadui wanaochukiana kutokana na tofauti za makabila lakini Uislamu umewaunganisha, hatimaye.

HABARI
DAR ES SALAAM

UKHTI FATIMA SS NA MWANDISHI WETU




# Masheikh waungana kuhimiza amani khutba za Ijumaa

Masheikh mbalimbali nchini wameungana katika khutba zao za Ijumaa wiki hii kuhimiza Waislamu na wananchi kwa ujumla kulinda na kutunza amani ya nchi na kujiepusha na vitendo vyote vinavyopelekea fujoi na machafuko katika taifa.

Utafiti uliofanywa na Gazeti Imaan kwa kuzungumza na masheikh na Waislamu wa kawaida na pia kupitia maudhui ya khutba zilizowekwa katika mitandaoi wiki hii unaonesha kuwa amani imehimizwa sana na masheikh wengi wamewaambia Waislamu kuwa amani ni neema kubwa na kila kitu kingine kinategemea amani.

Katika mtandaoi wa Youtube khutba nzima ziliwekwa zilizohimiza amani ilhali katika mitandao ya kijamiii kama Instagram, Facebook, WhatsApp na Twitter vipande vya video na sauti viliwekwa vikionya kuhusu uvunjifu wa amani.

Waislamnu waliambiwa kabla ya kuanzisha fujoi wakumbuke kuwa waathirika wakubwa watakuwa ni mama zao, vikongwe katika babu na bibi zao na pia watoto wadogo, ambao hawana hatia yoyote.

Baadhi ya masheikh wamewakumbusha wananchi matokeo ya fujo za Oktoba 29 ambapo watu waliuawa, mali za watu kuharibiwa na wananchi kulazimika kukaa ndani takriban wiki nzima wakishindwa hata kujitafutia riziki zao.

Masheikh, aidha walikumbusha namna Waislamu na watu wa dini nyingine waliposhindwa hata kwenda kwenye nyumba za ibada kuabudu kwa sababu ya hali ya machafuko iliyotawala kipindi hicho. Masheikh walionya kuwa kudai haki isiwe kisingizio cha kuvunja amani kwa sababu amani ni penye amani ndio mazungumzo ya kudai haki yanaweza kufanyika.

Waislamnu pia walionywa kuwa wasishabikie mambo ambayo hawajui undani wake kwani inawezekana sio haki pekee inayodaiwa bali kuna mipango ya hujuma kutoka ndani na nje ya nchi kwa sababu mbalimbali.

# Mkakati mpya wazinduliwa kuirejesha Tanzanite kwenye hadhi ya kimataifa

Serikali imezindua mkakati mahususi wa kufufua biashara ya Tanzanite na kuirudisha katika nafasi yake ya juu kwenye soko la dunia.

Akizungumza katika Kituo cha Tanzanite Mererani, Waziri wa Madini Anthony Mavunde alisema mpango huo unalenga kuimarisha usimamizi wa soko, kuboresha utambulisho wa kibiashara na kuimarisha mifumo ya biashara ya ndani kupitia Kituo cha Tanzanite.

Mavunde alisema Tanzanite imewahi kuingiza hadi Sh161 bilioni kwa mwaka, na kwamba sekta ya madini kwa sasa imefikia mchango wa asilimia 10.1 ya Pato la Taifa, juu ya matarajio yaliyowekwa kwenye Sera ya Madini ya 2009.

Alibainisha kuwa amechagua Manyara kama moja ya ziara zake za mwanzo kutokana na umuhimu wa Tanzanite kitaifa na kiuchumi kwa wakazi wa Mererani na Simanjiro, na hivyo kuhitaji kusikia maoni yao kabla ya hatua za mwisho za serikali.

Waziri huyo alikiri kuwepo kwa malalamiko kuhusu kushuka kwa bei, akisema thamani ya vito inategemea upekee na usimamizi madhubuti, na kwamba uzalishaji usio na mpangilio huporomosha bei.

Mpango mpya unajengwa juu ya nguzo tatu:

(1) Kuboresha chapa ya Tanzanite na kuirudisha kwenye minada ya kimataifa na maonesho ya vito.

(2) Kukamilisha na kuimarisha Kituo cha Tanzanite kama kitovu cha bei, ufuatiliaji na kodi.

(3) Kuanzisha mji maalum wa "Tanzanite City" utakaokuwa na miundombinu ya biashara, hoteli na huduma za usafirishaji.

Mavunde alisema serikali inalenga "kuhamisha masoko ya dunia" na kuyaweka Tanzania kwa kujenga mifumo ya uhakika ya biashara, ikiwemo malipo ya ndani ya saa 24 kupitia Benki Kuu.

Ili kuwajengea uwezo wafanyabiashara wa ndani, serikali inaanzisha skimu ya dhamana ya mauzo nje ili kuwawezesha kushindana na wanunuzi wakubwa wa kimataifa. Alionya pia dhidi ya magendo kupitia njia kama Rombo, akisema hatua za kisheria zitaendelea.

Ofisi za Madini za Mikoa zimeelekezwa kuwapanga wafanyabiashara kwa uwezo wa mtaji ili kuanzisha programu za kuwaendeleza kulingana na viwango vyao.

Akigusia ajira kwa vijana, Mavunde alisema vijana 291 tayari wamepatiwa leseni za uchimbaji, sambamba na dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha Watanzania wananufaika moja kwa moja na rasilimali za madini.

"We are here to lift Tanzanite back to the top," alisema. "Tutadhibiti biashara yake kwa uadilifu na kuhakikisha thamani yake inawaletea Watanzania maendeleo."




HABARI

DAR ES SALAAM

NA MUGINI SINGIRA

# Serikali yatoa msimamo Ulaya ikizuia misaada kwa Tanzania

Wakati Bunge la Umoja wa Ulaya (EU) likipitisha azimio la kuzuia fedha zilizopangwa kutolewa kwa Tanzania mwaka 2026, Serikali imeeleza kuwa, inafuatilia kwa karibu suala hilo na balozi wa Tanzania anayehudhuria mjadala huo akileta ripoti yake, watatoa taarifa.

EU imefikia uamuzi wa kuzuia fedha za msaada ilizopanga kuzitoa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Tanzania kutokana na mauaji yaliyotokea siku ya uchaguzi Oktoba 29, 2025 pamoja na mwendelezo wa ukiukwaji wa haki za binadamu.

Hivi karibuni, azimio hilo lilipitishwa kwa kura za 'Ndiyo' 539, kukiwa hakuna kura 'Hapana' iliyopinga azimio hilo huku wabunge 27 wa EU wakiamua kutopiga kura ama kuunga mkono au kupinga azimio hilo.

Umoja wa Ulaya ulipanga kutoa Euro 150 milioni (zaidi ya Sh400 bilioni) kwa Tanzania mwaka 2026 kwa ajili ya miradi ya maendeleo lakini umeeleza wasiwasi wake wa kuzorota kwa hali ya haki za binadamu na utawala wa sheria nchini.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mahmoud Thabit Kombo alisema jana kuwa, wanafuatilia kwa karibu mjadala huo na Balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji, Jestas Nyamanga anahudhuria majadiliano hayo.

Alisema watakapomaliza na kufanya uamuzi, Balozi Nyamanga ataandika ripoti yake, kisha Serikali itatoa kauli kuhusiana na kitakachoamuliwa kwenye kikao hicho cha Bunge la Umoja wa Ulaya.

"Tunafuatilia majadiliano hayo na Balozi Jestas Nyamanga yuko huko kama mwalikwa. EU




Bunge la Umoja wa Ulaya

wana haki ya kujadili chochote kwa sababu ni fedha zao, ni haki yao. Balozi wetu atatuleta ripoti kisha Serikali tutatoa taarifa," alisema Balozi Kombo.

Kuhusu fedha ambazo Tanzania itazikosa kutoka EU, Balozi Kombo alisema hadhani kama Tanzania ikizikosa fedha hizo, wananchi watalala njaa kwa sababu ina bajeti yake na vyanzo vingine vya mapato.

"Fuatilia huko mitandaoni ujue ni kiasi gani cha fedha tutakikosa...Sisi Watanzania hatutakufa kwa kukosa fedha hizo. Angalia wanatoa kiasi gani, kaangalie na bajeti yetu kwa mwaka, kisha fanya hesabu ni asilimia ngapi ya bajeti yetu," alisema Balozi Kombo.

Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/26 ni Sh56.49 trilioni zitakazotokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwamo vya ndani na nje ya nchi.

Hatua hiyo ya EU ni mwendelezo wa jumuiya ya kimataifa kueleza kuguswa na kilichotokea nchini katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 29 mwaka huu huku watu wakipoteza maisha wakati wa makabiliano na Jeshi la Polisi.



Pia, kulitokea uharibifu wa mali zikiwamo pikipiki, magari, vituo vya mafuta, nyumba za watu na ofisi za Serikali zilichomwa moto. Vituo vya mabasi yaendayo haraka (BRT) na miundombinu mingine iliharibiwa.

Katika mjadala huo, Bunge la EU lilieleza kusikitishwa na mauaji yaliyotokea huku likieleza uchaguzi haukuwa wa kidemokrasia kutokana na kukosekana kwa ushindani wa haki na kweli baina ya vyama vya siasa.

Bunge linalaani vikali matumizi ya nguvu ya mamlaka za Tanzania dhidi ya waandamanaji baada ya uliosababisha vifo na majeruhi.

Bunge hilo limeitaka Serikali ya Tanzania kuanzisha mazungumzo na upinzani, asasi za kiraia na wawakilishi wa waathirika ili kushughulikia mzozo huo na kuwezesha kufanyika kwa uchaguzi mpya wa kuaminika na wa uwazi.

Wabunge wa Bunge la Ulaya, pia wanalaani kukamatwa kiholela kwa watu, akiwamo kiongozi wa upinzani, Tundu Lissu ambaye hakushiriki mchakato wa uchaguzi na kufunguliwa mashtaka ambayo adhabu ni kifo, na wanazitaka mamlaka kumuachilia mara moja bila masharti.




MAKALA MAALUM

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Nini maana ya tume huru?

**Katika mjadala wa uchaguzi, neno "tume huru" limekuwa likitajwa mara kwa mara, lakini mara nyingi hutafsiriwa vibaya au kutumiwa kwa malengo ya kisiasa ili lisieleweke kikamilifu.**

Wapo wanaodhani kuwa tume huru ni ile isiyoitegemei Serikali kwa chochote, ikiwemo fedha; na wapo wanaodhani kuwa kule kuteuliwa kwa wajumbe na Rais ni ushahidi wa moja kwa moja kwamba tume hiyo si huru. Hizi ni dhana potofu zinazohitaji kuelezwa kwa uwazi ili wananchi wapate picha sahihi ya namna tume za uchaguzi zinavyofanya kazi duniani.

Kwanza, tume huru haimaanishi tume inayojitegemea kifedha bila ya mkono wa Serikali. Hakuna nchi duniani ambako tume ya uchaguzi au nyingineyo inajilipa, inajihudumia au inajitoa kwenye mfumo wa bajeti ya umma.

Fedha za tume katika mataifa yote; kuanzia India kwa mfano, Afrika Kusini, Ghana hadi Canada, hutoka kwenye Hazina ya Serikali na huidhinishwa na Bunge. Hii ni kwa sababu uchaguzi au tume ni shughuli ya kiserikali, inayogharimiwa na kodi za wananchi, si fedha binafsi au misaada isiyodhibitiwa.

Hata hivyo, ukweli muhimu ni kwamba bajeti ya tume lazima ilindwe kisheria ili kuzuia Serikali au chama chochote kuitumia kama fimbo ya kisiasa. Serikali isiwe na uwezo wa kuchelewesha, kupunguza au kuinyima tume fedha zake kwa sababu tu matakwa ya kisiasa hayajaridhiwa.

Katika mifumo bora, matumizi ya tume hupangwa mapema, hutangazwa hadharani, na Serikali inawajibika kutoa fedha hizo bila ubaguzi wala shinikizo. Huu ndio msingi wa tume huru: si chanzo cha fedha, bali namna fedha zinavyotolewa bila kuathiri uhuru wa maamuzi ya tume.

Pili, suala la uteuzi wa wajumbe wa tume limekuwa chanzo kingine cha mkanganyiko. Wapo wanaoamini kuwa endapo Rais anateua wajumbe, basi tume si huru. Ukweli ni kwamba katika karibu kila nchi inayoteua tume au inayoendesha uchaguzi wa kidemokrasia, Rais, Waziri Mkuu au chombo cha juu cha serikali huteua viongozi wa tume.

Hata hivyo, uteuzi pekee si kipimo cha uhuru wa tume. Kinachojenga uhuru ni: vigezo vya wazi vya uteuzi, uhakiki wa Bunge au chombo kingine, utamaduni wa kuheshimu katiba, na aina ya ulinzi wa ajira ambao wajumbe wanapewa ili wasiweze kuondolewa kirahisi kwa misingi ya kisiasa.

Mfano mzuri ni Tume ya Uchaguzi ya India (Election Commission of India). Wajumbe wake huteuliwa na Rais, lakini wana ulinzi wa kikatiba unaowazuia kuondolewa kiholela. Bajeti yao hutengwa mapema na Bunge, na Serikali haina mamlaka ya kuingilia mipango ya tume wakati uchaguzi unaendelea. Hii imeifanya India kutambulika kama moja ya nchi zenye mifumo thabiti ya uchaguzi duniani

Mfano mwingine ni Afrika Kusini, ambako tume huteuliwa na Rais lakini baada ya mapendekezo ya Bunge na ushirikishwaji wa vyama vya siasa. Bajeti yao inalindwa kisheria, na maamuzi makuu ya tume hayawezi kubadilishwa na serikali ya siku. Hata kama wagombea hawaridhiki na matokeo, mara nyingi hoja zao huangukia mahakamani badala ya kutuhumu tume moja kwa moja.

Hata katika nchi zilizoendelea kama Canada, wajumbe wa tume ya uchaguzi wanateuliwa na Waziri Mkuu, lakini wanafanya kazi bila kuingiliwa na chama tawala kwa sababu mfumo wa ulinzi wa kiutendaji ni madhubuti na wa muda mrefu.

Kwa hivyo, dhana ya tume huru haipaswi kupotoshwa na hisia au matokeo ya kisiasa. Uhuru wa tume unatokana na mfumo wa sheria, uwazi, uadilifu wa viongozi wake, ulinzi wa bajeti, na uwezo wa kufanya maamuzi bila kushawishiwa na serikali au vyama.

Na si suala la nani anateua, bali ni mazingira yanayolinda tume kufanya kazi kwa weledi na haki.

Katika muktadha huo, ni muhimu kwa wananchi kuelewa kuwa tume huru ni chombo cha kikatiba kinacholindwa na mfumo, si chombo kinachoishi kwa hofu ya matakwa ya kisiasa. Huu ndio msingi wa demokrasia ya kweli.

Afya
Pure Drinking water

"Afya"is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.

WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com






# Benki ya Maendeleo ya Afrika yatoa wito kwa uwekezaji wa sekta binafsi

Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dkt. Sidi Ould Tah, amesisitiza umuhimu wa kuhamasisha mitaji ya sekta binafsi ili kuziba pengo kubwa la ufadhili wa maendeleo barani Afrika, akibainisha kuwa rasilimali za umma pekee haziwezi kuhimili mahitaji ya bara.

Akizungumza katika ufunguzi wa Jukwaa la Uwekezaji la Afrika (Africa Investment Forum – AIF) 2025, alisema ajenda ya uwekezaji ya AfDB inajengwa juu ya mkakati mpana unaolenga kuongeza mtaji kupitia vyombo bunifu vya kifedha, kuleta mageuzi katika usanifu wa fedha barani Afrika, kuwekeza katika uwezo wa vijana na wanawake, na kuimarisha miundombinu itakayoongeza thamani ya rasilimali za bara.

Katika hotuba yake, Dkt. Tah alibainisha kwamba Afrika inahitaji zaidi ya dola trilioni 1.3 kila mwaka ili kufikia malengo yake ya maendeleo, hivyo ushiriki wa sekta binafsi ni hitaji lisilozuilika.

Morocco, mwenyeji wa mkutano huo, imerejea dhamira yake ya kuongeza uwekezaji wa sekta binafsi kufikia asilimia 66 ya uwekezaji wote wa taifa ifikapo mwaka 2035, kupitia mageuzi ya sera na mazingira rafiki kwa wawekezaji.

Mwaka huu, AIF inaonesha miradi 41 tayari kwa uwekezaji, ikijumuisha nishati jadidifu, miundombinu, uchumi wa kidijitali, kilimobiashara na viwanda. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018, jukwaa hili limevutia zaidi ya dola bilioni 225 katika nia ya uwekezaji, huku dola bilioni 32 zikiwa tayari zimefikia hatua ya financial close.

AfDB ina uhusiano mzuri na sekta ya benki za Kiislamu, ambapo kwa pamojan na Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB) zimekuwa zikijenga ushirikiano unaolenga kuunganisha maarifa, kuimarisha mbinu za tathmini na kutekeleza miradi yenye kuzingatia uadilifu, uwazi na misingi ya kimaadili. Ushirikiano huo, ulioimarika zaidi mwaka 2025, umejikita katika kusaidia nchi wanachama kupunguza hatari, kuimarisha uthabiti wa kiuchumi na kutekeleza miradi ya kijamii kwa njia shirikishi.

## AlHuda CIBE kuisaidia Somaliland kuendeleza sekta Benki za Kiislamu

Benki Kuu ya Somaliland (BoS) imeanza ushirikiano wa kimkakati na AlHuda Centre of Islamic Banking and Economics (AlHuda CIBE) wa Dubai, UAE, ili kuendeleza mfumo kamili wa benki za Kiislamu na soko la mitaji linalofuata Shariah nchini humo.

Mkutano wa mwanzo uliofanyika makao makuu ya BoS ulihudhuriwa na Bw. Muhammad Zubair, Mkurugenzi Mtendaji wa AlHuda CIBE, Gavana Bw. Abdinasir Ahmed Hirsi, Naibu Gavana Bw. Hamse A. Khaire, na Mkurugenzi wa Usimamizi wa Deni la Umma, Bw. Abdirahman Omar Ibrahim.

Gavana Bw. Hirsi alieleza azma ya BoS ya kuanzisha mfumo wa kifedha wa kisasa unaokamilika kwa Shariah na akatamka dhamira ya kuendeleza mfumo wa benki na kifedha unaokidhi 100% misingi ya Kiislamu. Mkurugenzi Mkuu Bw. Yasin Jama Axmed pia alisisitiza kujenga mazingira rafiki kwa maendeleo ya bidhaa za benki za Kiislamu na kukuza ujumuishaji wa kifedha pamoja na ukuaji wa uchumi.

Ushirikiano huu unahusisha utafiti wa kina, kuunda bidhaa za benki za Kiislamu, muundo wa utawala wa Shariah, na programu za mafunzo kwa wataalamu wa benki. Pia utalenga kuanzisha soko la mitaji la Kiislamu, ikiwemo muundo wa Sukuk kama chombo cha uwekezaji wa kiserikali na kibiashara.

AlHuda CIBE pia itasaidia kuendeleza bidhaa za kibiashara, za rejareja na SME, kuhakikisha taasisi za kifedha nchini zina mifumo ya kisasa, shindani, na inayoendana kikamilifu na Shariah. Bw. Muhammad Zubair alisisitiza kuwa soko la mitaji la Kiislamu na Sukuk ni muhimu kwa ukuaji wa sekta ya benki na fedha za Kiislamu.



## Nchi za Kiarabu-Afrika zasaka vyanzo vya fedha miradi ya kijamii

Mkutano wa kwanza wa nchi za Kiarabu-Afrika kuhusu Ufadhili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali uliofanyika Alhamisi iliyopita katika INSEA, Rabat, umehimiza kuunda mifumo mipya ya kifedha ili kuongeza athari za miradi ya kijamii na kuimarisha ushirikiano kati ya Afrika na dunia ya Kiarabu.

Wahudhuriaji walikubaliana kuwa ingawa zana zilizopo kama uwajibikaji wa makampuni kijamii (CSR), mfuko wa pamoja (crowdfunding), na fedha za Kiislamu (zaka, sadaka) zina mchango, bado hazitoshi kufikia lengo la athari kubwa za kijamii.

Mkutano uliitaka kuanzishwa kwa mifumo ya kifedha inayobadilika, bunifu, na inayoweza kupita mipaka ya michango ya jadi na ruzuku.

Wazungumzaji walisisitiza umuhimu wa kuunda majukwaa ya kidijitali yenye mchanganyiko wa rasilimali za umma, uwekezaji binafsi unaolenga athari za kijamii, na ushiriki wa wananchi. Pia walijadili fursa za Social Impact Bonds, zana zinazoruhusu wawekezaji binafsi kusaidia miradi ya




# Mtaalamu: Fedha za Kiislamu zilitangulia ESG, Dunia inaiga sasa

Mtaalamu Mohammad Ali Allawalla aliyebobea katika huduma za kifedha za Kiislamu ameieleza sekta hiyo kuwa tayari ilikuwa imejikita katika misingi ya maadili, uwazi na uendelevu—misingi ambayo leo dunia inaifahamisha kama ESG—hata kabla ya mfumo huo kupewa uzito katika masoko ya fedha.

Akizungumza na mwandishi Mahir Haneef katika makala iliyochapishwa Novemba 25 na News of Bahrain, mtaalamu huyo ambaye ni afisa mwandamizi wa Benki ya Standard Chartered, amesema kuwa "mfumo wa fedha za Kiislamu haukuhitaji ESG kuonekana wa maadili; misingi yake imekuwa ikiongozwa na mafunzo ya kuhakikisha uwajibikaji wa kijamii na kiuchumi tangu mwanzo."

ESG—kifupi cha Environmental, Social and Governance—ni mfumo unaopima kiwango cha maadili, uendelevu na uwazi wa taasisi za kifedha na kampuni. Unachunguza athari za shughuli za kibiashara katika mazingira, jamii, na namna uongozi unavyodhibitiwa.

Mtaalamu huyo amesema kuwa benki na taasisi za Kiislamu zimekuwa zikiweka vikwazo kwa shughuli zinazoathiri jamii na mazingira, kama vile biashara ya pombe, silaha, kamari na mafuta yenye madhara. Badala yake, zimekuwa zikihamasisha uwekezaji katika shughuli za kiuchumi zinazochochea ustawi wa jamii, jambo ambalo linalingana moja kwa moja na malengo ya ESG.

Akielezea mwenendo wa sasa wa soko, mtaalamu huyo amesema kumekuwepo na kuongezeka kwa hamu ya kimataifa kwa bidhaa kama Sukuk endelevu, ambapo wawekezaji wanazipendelea zaidi kutokana na hadhi yake ya kuhusisha uendelevu wa kijamii na kimazingira. Sukuk hizi zimepata mwamko mkubwa kuliko zile za kawaida, ikiashiria mabadiliko ya fikra kuhusu uwekezaji wenye athari chanya.

Aidha, mtaalamu huyo anabainisha kuwa ujio wa teknolojia ya kifedha (fintech) umefungua fursa mpya kwa wateja wengi—hasa vijana na walio maeneo ambayo huduma za kibenki zilikuwa adimu—kuchangamkia bidhaa za Shariah. Hata hivyo, anatahadharisha kuwa changamoto za uwazi, usalama wa data na uhakiki wa uhalali wa kidini zinahitaji ushirikiano mpana kati ya wataalamu wa Shariah na wabunifu wa teknolojia.

Kwa mujibu wa maoni yake, mafanikio ya sasa ya ESG si jambo jipya kwa sekta ya fedha za Kiislamu; bali ni ulimwengu unaoanza kutambua thamani ya kanuni ambazo mfumo huo umeziweka mbele kwa miongo kadhaa—uadilifu, usawa, uwazi na manufaa ya kijamii.

## Malaysia kuongoza mageuzi kidijitali huduma za kifedha za Kiislamu?

**Malaysia ipo kwenye nafasi ya kipekee kuongoza mageuzi ya kidijitali katika huduma za kifedha za Kiislamu, kwa mujibu wa makala iliyoandikwa na Hugh Harsono kwenye tovuti ya HackerNoon Novemba 26, 2025.**

**Harsono anabainisha kwamba uzinduzi wa benki ya kwanza yenye nguvu za AI nchini, Ryt Bank, unaashiria jitihada za Malaysia kukuza ekosistimu yake ya kifedha ya kidijitali, sambamba na kuanzishwa kwa Malaysian Blockchain Infrastructure (MBI) mnamo Aprili 2025. Hatua hizi zinathibitisha kuungwa mkono na serikali katika mustakabali wa kidijitali wa kifedha.**

**Sababu kadhaa zinatofautisha Malaysia na kufanya nchi hiyo kuwa kiongozi wa mageuzi ya kidijitali ya fedha za Kiislamu. Kwanza, Malaysia ina nafasi ya kijiografia muhimu karibu na Indonesia, nchi yenye idadi kubwa zaidi ya Waislamu duniani, na pia inaunganishwa na nchi zinazoendelea kiuchumi kama Thailand, Vietnam, China na India. Harsono anasema hii inafanya Malaysia kuwa kivutio cha kimataifa kwa miradi ya kifedha ya kidijitali.**

**Pili, Malaysia inachangia kimsingi katika masoko ya fedha za Kiislamu, ikiwa na mifumo thabiti ya utawala na maelekezo ya Shariah kupitia International Islamic Financial Centre (MIFC) Leadership Council na Sharia Advisory Council (SAC) ya Benki Kuu ya Malaysia. Mfumo huu una kuhakikisha kwamba bidhaa zote za kifedha zinazingatia kanuni za kidini, jambo linalotoa msingi thabiti wa kuunganisha fintech ya kidijitali na fedha za Kiislamu.**

**Tatu, Malaysia ina idadi kubwa ya raia walio na uelewa wa kidijitali (digital natives), hasa vijana wa kizazi cha Gen Z, ambao wanachukua huduma za kidijitali kila siku. Sekta ya malipo ya kidijitali tayari inaongeza ushawishi mkubwa katika maisha ya Wamalaysia. Hii inatoa fursa ya kuchanganya teknolojia ya AI na huduma za kifedha za Kiislamu kwa urahisi mkubwa.**

**Nne, Malaysia ni kiongozi katika masoko ya sukuk, na karibu 40% ya amana za benki zipo kwenye benki za Kiislamu. Kuingiza mifumo ya kidijitali katika sukuk na zaka inaweza kupanua huduma, kupunguza gharama na kurahisisha ukaguzi wa uwazi. Aidha, wajasiriamali wadogo na wa kati (MSME) wanapata fursa ya mikopo ya kidijitali, ufadhili wa biashara, na tokenization ya minyororo ya usambazaji, huku wakichangia 40% ya Pato la Taifa (GDP).**

**Harsono pia anataja changamoto, ikiwemo upatikanaji usio sawa wa zana za kidijitali na hofu ya usalama wa data kwenye huduma ya kitaifa ya utambulisho (MyDigital ID), ambapo chini ya 10% ya Wamalaysia walio na sifa wamejisajili hadi Julai 2025. Hata hivyo, anasisitiza kuwa ikiwa changamoto hizi zitashughulikiwa, Malaysia inaweza kushikilia nafasi ya kimsingi katika soko la fintech ya Kiislamu duniani, linalokadiriwa kufikia dola bilioni 179 ifikapo 2026.**

**Soma zaidi hapa: https://hackernoon.com/why-**



# Utafiti: Unyanyasaji wa kutisha kwa Wanawake Waislamu kwenye treni Uingereza

Utafiti mpya mkubwa umeonyesha kiwango cha kutisha cha unyanyasaji, hofu na ubaguzi wanaokutana nao wanawake Waislamu wanapotumia usafiri wa umma nchini Uingereza.

Ripoti hiyo, iliyotolewa na Muslim Census kwa ushirikiano na Muslims in Rail, na kuchapishwa katika tovuti ya 5Pillars ya Uingereza imeelezwa kuwa ndiyo uchunguzi mpana zaidi kuwahi kufanywa kuhusu uzoefu wa Waislamu kwenye usafiri wa umma.

Utafiti uliowahusisha Waislamu 1,155 kutoka maeneo mbalimbali ya Uingereza kati ya Novemba 9–20, 2025 umebainisha kuwa wanawake Waislamu wana uwezekano wa mara tano zaidi kuhisi kutokuwa salama wanapotumia treni, basi au London Underground kuliko wanawake wengine nchini.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, 45.3% ya wanawake Waislamu walisema wanahisi kutokuwa salama wakisafiri, ikilinganishwa na asilimia 8 tu ya wanawake kwa ujumla. Zaidi ya hilo, 34.3% wamewahi kushuhudia au kushambuliwa kwa maneno ya kibaguzi au chuki dhidi ya Uislamu wakiwa safarini. Hofu hii imesababisha 69.4% kubadili ratiba zao za usafiri, kuacha kuvaa vazi la Kiislamu fulani, au kutumia taksi kwa gharama zao binafsi.

Utafiti umeonyesha kuwa matukio mengi hayaripotiwi; ni 12.5% tu ya unyanyasaji unaofikishwa kwa mamlaka. Zaidi ya 69% ya wanawake walisema hawana imani kuwa polisi au mamlaka zingechukua malalamiko yao kwa uzito.


Katika nyakati za misukosuko ya kisiasa au matukio ya makundi ya mrengo mkali wa kulia, karibu 96% ya wanawake Waislamu walisema wanahisi kutokuwa salama zaidi, huku wengine 90% wakibadili mpango wao wa safari.

Muslims in Rail walisema matokeo haya yanathibitisha ongezeko la chuki dhidi ya Waislamu kwenye usafiri wa umma na kutaka hatua za haraka zinachukuliwa. Walisema hakuna mwanamke anayepaswa kusafiri kwa hofu "kwa sababu tu ya jinsi anavyoonekana."

Ripoti hii imetolewa wakati ambapo visa vya chuki dhidi ya Waislamu vinaongezeka nchini. Takwimu zinaonyesha kwamba Waislamu sasa ni wahanga wa 44% ya uhalifu wa chuki za kidini, licha ya kuwa chini ya 7% ya idadi ya watu. Ongezeko hili limechochewa na propaganda za mrengo mkali wa kulia, vurugu za majira ya kiangazi 2024, na chuki iliyoendelea kushamiri tangu vita vya Gaza kuanza mwaka 2023.

Muslim Census na Muslims in Rail wanashirikiana na taasisi za usafiri na polisi kutaka mafunzo maalum ya kukabiliana na chuki dhidi ya Uislamu na hatua za kuongeza usalama kwa wasafiri wote.

UKHTI FATIMA SS



# Ukatili wa Wabudha kuwalenga Waislamu washtua Dunia

Gazeti la The Guardian la Uingereza limeonya kuhusu kuibuka kwa misimamo mikali ya Wabudhi katika nchi kadhaa za Asia, hali inayowafanya Waislamu kuwa miongoni mwa waathirika wakubwa wa sera na siasa za chuki zinazofichwa nyuma ya kauli za "kulinda Ubudha na taifa."

Kwa mujibu wa The Guardian, nchini Sri Lanka na Myanmar, baadhi ya maaskofu na watawa wa madhehebu ya Theravada wamegeuka kuwa viongozi wa harakati za kitaifa zenye chuki dhidi ya makundi madogo ya kidini, hususan Waislamu.

Nchini Sri Lanka, makundi kama Bodu Bala Sena (BBS) yamekuwa yakitumia lugha za uchochezi dhidi ya Waislamu, yakihamasisha umma "kutolala" wakidai Ubudha uko hatarini. Matokeo yake yamekuwa mashambulizi ya umma dhidi ya familia na biashara za Kiislamu, kuchomwa kwa nyumba na hata misikiti, huku polisi wakilaumiwa kwa kushindwa kuwalinda raia.

The Guardian inaripoti simulizi za Waislamu waliovamiwa majumbani kwao, mali zao kuchomwa moto na majirani zao wa Kibudhi waliowajua kwa miaka mingi, wakichochewa na hotuba za watawa wenye ushawishi wa kisiasa. Watawa hao, wanaovikwa heshima kubwa kijamii, wanatajwa kutumia mavazi yao ya manjano kama kinga wakati wakihamasisha chuki dhidi ya Waislamu na kuwasilisha Uislamu kama "tishio la ndani" kwa utambulisho wa taifa.

Hali kama hiyo imeonekana Myanmar, ambako watawa kama Ashin Wirathu wamehusishwa moja kwa moja na kampeni za chuki na ukatili dhidi ya Waislamu wa Rohingya, waliouawa, kubakwa na kulazimishwa kukimbia nchi.

## Kuwa na wake wengi jela miaka 10 jimbo la Assam, India!

**Wabunge wa jimbo la Assam, kaskazini mashariki mwa India, wamepitisha sheria mpya inayokataza ndoa za wake wengi—hatua inayotajwa na serikali ya chama cha BJP kama "ulinzi wa wanawake" lakini wakosoaji wanasema inalenga Waislamu.**

**Sheria hiyo, Assam Prohibition of Polygamy Bill 2025, inafanya kuoa wake wengi wakati bado una ndoa halali kuwa kosa la jinai linaloweza kupelekea kifungo cha hadi miaka saba. Kwa mujibu wa tovuti ya 5Pillars ya Uiongereza, Mtu anayeficha kuwepo kwa ndoa ya awali na kuoa tena anaweza kufungwa hadi miaka kumi pamoja na faini.**

**Sheria inawawajibisha pia wanaosaidia ndoa hizo, wakiwemo viongozi wa vijiji, maimamu, na hata majaji wanaohalalisha ndoa za Kiislamu; wanaweza kufungwa hadi miaka miwili au kutozwa faini ya rupia 100,000.**

**Ingawa Uislamu unaruhusu wanaume kuoa hadi wake wanne kwa masharti ya uadilifu kamili, wakosoaji wanasema muswada huu unakiuka uhuru wa kidini. Mbunge huru Akhil Gogoi alisema sheria hii inavunja Kifungu cha 25 cha Katiba ya India kinacholinda uhuru wa kuabudu.**

**Chama cha AIUDF, chenye uungwaji mkubwa kutoka jamii ya Waislamu wa Assam, kilisema muswada huo unaweza kutumiwa vibaya na umelenga wazi kutikisa sheria za Kiislamu. Marekebisho yao yalikataliwa bila hata kura ya wazi.**

**Wachambuzi wanasema sheria hii ni sehemu ya msukumo mpana wa BJP kusukuma Uniform Civil Code (UCC), hatua inayolenga kuondoa sheria za dini mbalimbali na kuweka kanuni moja ya kiraia—ambayo inaonekana kuhatarisha haki za makundi ya wachache.**

## KUTOKA KWA MHARIRI

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

# Misingi ya umoja wetu inatetereka, tuchukue hatua

Tumefurahishwa na hatua ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuunda Tume Huru ya Uchunguzi wa matukio ya uvunjifu wa amani kufuatia vurugu zilizotokea wakati wa Uchaguzi Mkuu mnamo Oktoba 29 na 30 mwaka huu.

Tunaamini hatua hiyo itajenga maridhiano, kuponya majeraha ya kisiasa na kuimarisha msingi wa amani na umoja wa kitaifa. Hii inadhihirisha kwamba amani na umoja ni tunu mbili zinazotuunganisha Watanzania. Hivyo kila mwananchi ana wajibu wa kuwa mlinzi wa amani na umoja wa kitaifa.

Sisi, gazeti la Imaan tunatoa pole na rambirambi kwa wale wote walioathirika kwa namna moja ama nyingine na vurugu zilizotokea wakati na baada ya uchaguzi. Ili yale yaliyotokea wakati wa uchaguzi yasijirudie, tunasisitiza kusameheana, kuheshimu utu wa kila mmoja na kuimarisha mshikamano wa kijamii.

Katika kusisitiza umuhimu wa kusameheana, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "...na wanazuia ghadhabu na wenye kusamehe watu. Na Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao ihsani." 3:134]. "Na atakayevuta subira na akasamehe, hakika hilo bila shaka ni katika mambo ya kuazimiwa." [Qur'an, 42:43].

Kwa mantiki hiyo, ni vyema wito wa msamaha na maridhiano uendelee kutolewa kwa makundi yote wakati huu ambapo Tume ya Uchunguzi inaendelea na majukumu yake, ili kujenga upya imani ya kitaifa na kuondosha chuki na vifundo kati yetu. Maridhiano ni msingi muhimu katika kuponya tofauti zilizojitokeza wakati na baada ya uchaguzi.

Rais Samia, mara kwa mara amekuwa akisisitiza kwamba Taifa haliwezi kuendelea bila maridhiano ya kweli. Kutokana na hilo, Rais amehimiza Watanzania kupinga kauli za uchochezi, kukataa propaganda zinazoleta mgawanyiko, na kujikita katika mazungumzo na mijadala yenye tija na staha. Halikadhalika, watu wa kada mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini wametoa wito wa kusameheana na kufanya maombi ya kitaifa kwa ajili ya kuiombea nchi amani na kurejesha imani kati ya wananchi na Serikali.

Uislamu, ambao ni mfumo kamili wa maisha ya wanadamu unahimiza kusameheana na kufanya mazungumzo na majadiliano baina ya watu ili kuondoa migogoro na mitanziko kutatuliwa. Majadiliano makini na mazungumzo thabiti ni ushahidi wa kupevuka, kuboreka na kuimarika kwa jamii. Na kutofautiana ni katika utaratibu wa maisha.

Watanzania tumelelewa katika misingi ya umoja, upendo na mshikamano, hivyo ni lazima tufungue ukurasa wa mazungumzo na majadiliano na kila upande kwa lengo la kufikia haki na kuondoa migogoro, kueneza utulivu na kuleta suluhu endelevu.

Watu makini na werevu ni wale wanaovumiliana, kuheshimiana, na kufanya mazungumzo kwa mantiki, mawazo chanya ya kina na kwa kuzingatia maadili. Kufanya hivyo kunayapa majadiliano nafasi muhimu katika kuleta maridhiano ya kitaifa.

Afya
Pure Drinking water
"Afya"is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.
WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com




MAKALA MAALUM



NA SHEIKH SEIF RUGA

# Mafungamano ya amani na haki katika Uislamu

Hakika fadhila na hisani za Allah kwa wanadamu ni kubwa zisizo na ukomo wala mipaka, na neema zake haziwezi kuhesabiwa wala kuandikwa. Miongoni mwa neema kubwa zaidi za Allah ni amani na utulivu. Hizi ni nguzo muhimu za maisha na miongoni mwa mahitaji ya lazima kabisa kwa kila binadamu na hata viumbe wengine wa mwituni na baharini.

Uislamu unahimiza kwa hali yoyote ile kuyalinda mambo matano ya lazima, ambayo sharia zote za mbinguni zimekubaliana juu ya umuhimu wake. Mambo hayo ni dini, nafsi, akili, heshima na mali. Mambo haya hayawezi kulindwa ikiwa amani na utulivu vitatoweka.

Wanazuoni wa Kiislamu wameielezea amani kuwa ni 'Hali ya mtu binafsi au jamii, ndani ya taifa au nje yake kuhisi utulivu wa maisha na kuondolewa sababu zote za hofu.' Imam Ghazali (Allah amrehemu) ameweka wazi kwamba, kusimama kwa dini kunategemea kusimama kwa dunia..., na utaratibu wa dini una misingi yake katika elimu na utekelezaji wa ibada, lakini elimu na ibada haziwezi kufanyika bila ya kuwa na afya, uhai, na mahitaji muhimu kama makazi, mavazi, chakula na amani.

Tangu kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu Oktoba 29 mwaka huu nchi yetu inapitia kipindi kigumu katika mambo matano ambayo dini za mbinguni zimekubaliana kuyalinda. Akili na heshima ndiyo mambo ya mwanzo kushambuliwa hata kabla ya siku ya maandamano, ambapo wezi wa akili na wavunjifu wa heshima za watu walianza kuharibu akili za baadhi ya watu kupitia mitandao ya kijamii.

Amani ya akili na fikra ni muhimu sana kama ilivyo amani ya roho na mali. Kama ambavyo roho na mali vina wezi wake ambao wanaweza kuviiba, vivyo hivyo akili pia zina wezi. Hawa ni watu wanaoharibu fikra za watu. 'Wezi wa akili' ni hatari zaidi kuliko wale wanaoiba mali.

Siku mbili baada ya kufanyika uchaguzi (Oktoba 31, 2025) dini yetu iliathirika, kwani siku hiyo Waislamu katika misikiti mingi walishindwa kutekeleza ibada ya sala ya Ijumaa kwa sababu ya ukosefu wa amani. Mali na roho za watu ndiyo zilizoathirika kwa kiwango kikubwa sana.

Bila shaka kila mmoja wetu amepata somo la umuhimu wa amani. Wahenga walisema: "Kuielezea hali kwa vitendo hufahamika zaidi kuliko kuielezea kwa maneno." Amani ikipotea mzunguko wa maisha husimama na hivyo kurudisha nyuma maendeleo. Kwa kuzingatia hilo, Nabii Ibrahim (amani imshukie) aliwaombea watu wa Makka dua hii: "Na aliposema Ibrahim: Ee Mola wangu Mlezi! Ufanye mji huu uwe na amani, na uwaruzuku watu wake matunda..." [Qur'an, 2:126].

Katika vurugu za uchaguzi, vyakula vilipanda bei na kufikia nyanya moja kuuzwa Sh2,000 huku hofu ikitawala kutoka eneo moja hadi nyingine. Allah Mtukufu amewaonya watu wanaoikana neema ya amani kwa kusema: "Na Mwenyezi Mungu amepiga mfano wa mji uliokuwa na amani na utulivu, riziki yake ikiufikia kwa nafasi kutoka kila mahali. Lakini ukazikufuru neema za Mwenyezi Mungu; kwa hivyo Mwenyezi Mungu akauvika vazi la njaa na hofu kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyafanya." [Qur'an, 16:112].

Vitabu vyote vya mbinguni vimekuja kubainisha haki, uadilifu na tabia njema, na kukataza dhuluma, ukandamizaji na tabia mbaya. Allah anasema: "Na kwa haki tumeiteremsha (Qur'an), na kwa haki imeteremka..." [Qur'an, 17:105]. Lakini Uislamu unakataza kudai haki kwa wakati iwapo kutakuwa na mazingira ya umwagikaji damu, ili kuchunga maslahi ya roho za watu.

Mkataba wa Hudaibiya uliojiri baina ya makafiri wa Makka na Mtume wa Allah katika mwaka wa sita Hijriya unathibitisha hili. Mtume alitoka Madina na Masahaba wapatao 1500 kwa ajili ya kutekeleza ibada ya Umra Makka, lakini alipofika Hudaibiya makureish (makafiri) walimzuia.

Baada ya majadiliano mazito, pande zote mbili zilisaini mkataba wa amani wenye vipengele vingi vinavyowakandamiza Waislamu. Hali hii iliwafanya Masahaba kupinga mkataba huo, lakini Mtume aliwasihi kukubali vipengele hivyo ili kuzuia umwagaji damu. Mtume alimwamuru mwandishi wake kuandika katika hati ya mkataba: "Haya ndiyo makubaliano yaliyoafikiwa baina ya Muhammad, Mtume wa Allah, na makafiri wa Makka."

Lakini makafiri walipinga kuandikwa 'Muhammad Mtume wa Allah' badala yake iandikwe 'Muhammd bin Abdillah'. Ili kulinda damu za Waislamu, Mtume alikubali matakwa yao, lakini akawaambia: "Mimi ni Mtume wa Allah hata kama mnapinga hilo kuandikwa."

Huu ni ushahidi kuwa haki ndiyo msingi wa amani, lakini katika mazingira ya umwagaji damu ni vema kuacha kudai haki kwa wakati ili kulinda damu za watu, lakini siyo kuinyamazia. Ni muhimu kukumbusha haki hiyo ili anayeizuia ajue kuwa ipo kama Mtume wa Allah alivyofanya.


Allah anasema: "Tuliwaandikia Wana wa Israili ya kwamba aliyemuua mtu ambaye hakuua au hakufanya uharibifu katika nchi, basi ni kama amewaua watu wote. Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote..." [Qur'an, 5:32]. Kulinda roho za watu kuna thamani kubwa katika dini ya Uislamu kuliko kitu kingine chochote. Mwaka wa nane Hijriya (miaka miwili mbele), Mtume alirejea katika mji wa Makka kwa amani huku akisema: "Na sema: haki imefika, na batili imetoweka. Hakika batili lazima itoweke!" [Qur'an, 17:81].



# NASAHA ZA WIKI



NA YUSUFU AMINI
0787 503 085



# Unaposaidia yatima usisahau watoto wa nduguzo

Kuna fadhila nyingi na malipo makubwa kwa mwenye kuwasaidia yatima wasiojiweza. Allah Mtukufu, kwa hekima yake amejaalia yatima waishi katikati yetu ili tupate thawabu na fadhila, ambazo hazipatikani popote isipokuwa kwa kuwasaidia yatima.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehema na amani iwe juu yake) amesema: "Mimi na mwenye kumlea yatima tutakuwa hivi Peponi (akaashiria kidole cha shahada na cha katikati kwa pamoja kisha akaviachanisha baina yake)." [Bukhari]. Katika hadith nyingine amesema: "Mwenye kuweka mkono wake kwenye kichwa cha yatima kwa upole, Allah humuandikia jema kwa kila unywele aliougusa kwa mkono wake." [Ahmad].

Ijulikane wazi kuwa, kuwalea yatima ni aina ya hisani ambayo mtu yeyote (Muislamu au asiye Muislamu) anaweza kufanya. Isivyo bahati, Waislamu wengi katika zama zetu hizi wameghafilika na kutekeleza jambo hili muhimu katika Uislamu. Kuwalea yatima siyo tu ni ibada inayoweza kutatua changamoto mbalimbali kwenye maisha yao, bali pia ni njia ya kuvuna thawabu nyingi kutoka kwa Allah.

Licha ya kuwapo Waislamu wengi wenye uwezo wa kimali katika jamii zetu, inashangaza kuona wapo watoto wengi yatima ambao hawana watu wa kuwasaidia kupata elimu na mahitaji muhimu ya binadamu, jambo linalofanya maisha yao kuwa magumu zaidi na hivyo kupata hisia za huzuni ya kupoteza wazazi wao.

Kukosekana kwa juhudi za pamoja baina ya wanafamilia kunatajwa kuwa ni kikwazo kikuu katika kukabiliana na changamoto hii. Ukifanya utafiti mdogo kuhusu maisha ya yatima hapa nchini, utabaini wengi wao wanaishi kwenye vituo maalum vya kulelea yatima. Laiti kila mmoja wetu angechukua yatima mmoja na kuishi nae nyumbani kwake, ni wazi vituo vya kulelea yatima vingekuwa vichache mno.

Mtume Muhammad (rehema na amani iwe juu yake) aliishi na yatima nyumbani kwake na wala hakuwafanya kuwa watumishi wake wa ndani, wala kuwatenga kwa kuwahifadhi kwenye nyumba maalum kama tufanyavyo sisi leo.

Katika mafundisho ya Uislamu, mtoto anapofiwa na wazazi wake jukumu la kumlea linabaki kwa wanafamilia (kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na sharia) na siyo kumpeleka kwenye kituo cha kulelea yatima au watoto waishio katika mazingira magumu.

Huu ndiyo ulikuwa mwenendo wa Mtume na Masahaba (Allah awaridhie wote), kama anavyobainisha Mwenyezi Mungu: "Na wanalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini na mayatima na mateka." [Qur' an, 76:8].

Inastaajabisha kuona kuwa, siku hizi baadhi ya familia hazipo tayari kulea watoto wa ndugu zao wanaopitia changamoto mbalimbali, ikiwamo wazazi wao kufariki. Waislamu tumesisitizwa kuwalea yatima kwa moyo wa mapenzi, huruma na kuwapa mahitaji yao ya msingi, kuanzia chakula, elimu, malazi, sambamba na kuwarekebisha tabia na kuwafunza maadili mema.

Katika hili, wote tunapaswa kubadilika kwa kurudisha utamaduni wa zamani wa kulea watoto katika mfumo wa kifamilia. Tujenge utamaduni wa kutoa chochote tulichojaaliwa kuwasaidia yatima.

Serikali, taasisi na mashirika binafsi yameanzisha vituo vingi vya kulea yatima kama njia mbadala, lakini kimsingi watoto wanapaswa kulelewa na familia zinazowazunguka – ima ndugu zao wa damu au jamaa wa karibu.

Kwa maneno mengine, nyumba au vituo vya kulea yatima ni suluhisho la mwisho kwa ajili ya kuwatunza watoto pindi hatua nyingine zinapokwama, kwani wajibu wa kulea watoto na kuwatunza ni wa baba, mama na ndugu wa karibu wa familia.

Nihitimishe kwa kutoa wito kwa watu binafsi, taasisi na jumuiya mbalimbali kutumia sehemu ya faida katika shughuli zao kuwasaidia yatima ili kupata thawabu kwa Mwenyezi Mungu. Ni muhimu kuzingatia hilo kwa sababu, mtu hajui ni aina gani ya ibada ambayo akiifanya itapelekea kupata fadhila za Mwenyezi Mungu na hatimaye kuingia Peponi.

Mtu asidanganyike na wingi wa amali zake njema kwa kuona kuwa zinatosha kumuingiza Peponi. Siku ya Kiyama watu wataingia Peponi kwa rehema na fadhila za Allah Mtukufu kupitia njia zake, yaani sababu zinazopelekea kupata fadhila hizo, ikiwamo kuwalea na kuwatunza yatima.

Ni kwa sababu hiyo, Mtume (rehema na amani ya Allah iwe juu yake) amesema: "Amali za mtu hazitamuingiza Peponi (Siku ya Kiyama)." Masahaba (wakasema): "Hata wewe ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu." Akasema: "La! Hata mimi, isipokuwa Mwenyezi Mungu atanimiminia rehema zake." [Bukhari na Muslim].

MUSSA IMANI
SHEHA,
ZANZIBAR
0773 181 494



# ZAINAB BINT JAHSH

# Mke wa Mtume

## VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

**Wiki iliyopita tulianza kuangalia kisa cha mmoja wa wake wa Mtume, Zainab bint Jahsh (Allah amridhie). Ukiacha nasaba yake, tulianza pia kuangalia kisa chake kilichopelekea hadi kuolewa kwake na Mtume, ikiwa ni amri ya Mwenyezi Mungu ili kuondosha itikadi kwamba, mtoto wa kulea ni kama mtoto wa kumzaa.**

### Qur'an yawajibu wanafiki

Baada ya Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) kumuoa Zainab, wanafiki - kama kawaida yao - walisema sana, "O! Muhamad ameharamisha kuwaoa wake walioachwa na watoto wa kulea, lakini mbona yeye amemuoa mke wa mwanawe Zaidu, inakuwaje?!"

Ndipo Mwenyezi Mungu akawajibu kwa kusema: "Muhammad si baba wa yoyote katika vijana wenu, lakini yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa Mitume..." [Qur'an, 33:40].

Katika aya nyingine Qur'an inasema: "...na wala Allah hajajaalia wanenu wa kulea kuwa watoto wenu wa kuzaa. Hayo ni maneno yenu muyanenayo kwa vinywa vyenu (tu), ma Mwenyezi Mungu husema kweli naye huongoza njia ya sawa." [Qur'an, 33: 4].

Aya hizi zinawataka watu kuelewa kwamba, Zaidu si mtoto wa Mtume wa kumzaa kwani wakati huo watoto wa Mtume wanaume walishafariki. Na kwa hali hiyo, hakuna uharamu wowote Mtume kumuoa Zainab, aliyekuwa mke wa Zaidu, mwanawe wa kumlea.

### Utukufu na nafasi yake

Naam, basi Allah akamuozesha Mtume, bi Zainab (Allah amridhie). Alimuoa bila ya walii wala shahidi. Na kwa hilo, akijifakharisha sana mbele ya wake wenziwe, mama wa Waislamu, kama Anas (Allah amridhie) alivyomnukuu akiwaambia: "Nyinyi mumeozeshwa na mawalii wenu, lakini mimi Allah amenioza (kwa tamko lake) kutoka Arshi yake!"

Anasema Aisha (Allah amridhie): "Allah amrehemu Zainab, kwa hakika amepata utukufu mkubwa duniani ambao ni nadra kupatikana. Ameozeshwa na Allah, ambapo Qur'an imetoa tamko rasmi la ndoa yake. Na Mtume ametuambia sisi, 'Itakayekuwa rahisi kukutana nami kwa haraka ni atakayewazidi nyote kwa utoaji sadaka.'"

Kauli hii ya Mtume ilikuwa na ishara kwamba, Zainab ndiye atakayemfuatia Mtume kufa baada yake. Hili lilitimia hili kwani alikufa mwaka wa 20 hijriya kabla ya wakeze wote.

### Zainab mjasiriamali

Zainab (Allah amridhie) alifanya kazi nyingi za mikono zifanywazo na wanawake kama vile kushona, kufuma na kusuka. Pia, alitumia kipato chake kutoa sadaka na kuwasaidia jamaa zake. Vilevile, alijitahidi sana kwa ibada mbalimbali, zikiwemo kuswali, kufunga, dhikr na kusoma Qur'an.

Inasemekana kwamba, Umar alimpelekea Zainab dirhamu elfu 12 kama alivyoidhinisha kwa wake wengine wa Mtume, naye akazichukua na kuzigawa zote kwa wenye shida, mayatima na wajane. Kisha Zainab akamuomba Allah usimfikie tena mgao wa Umar kama huo mara nyingine. [Taz. Rijal wa nisaa hawla rasoul uk 116].

Katika kuelezea utukufu wake aidha, Aisha (Allah amridhie), anasema: "Sikupatapo kumuona mwanamke mwenye dini nzuri, na mchamungu zaidi, na mkweli zaidi, na mshughulikiaji zaidi wa familia yake, na mwenye uaminifu zaidi kuliko Zainab [Rijaal wa nisaa hawla rasoul uk.116].

Kwa upande wa elimu, Zainab hakuwa nyuma. Alipokea hadith nyingi kutoka kwa Mtume, naye akawafundisha wakina Muhamad bin Abdillah bin Jahsh (mtoto wa kaka yake), Ummu Habiba bint Abi Sufiyan (mke mwenziwe), Zainab bint Abii Salama, Kulthoum bint Almustwalaq na wengine wengi.

### Kifo chake

Ilipofika mwaka wa 20 Hijriya katika ukhalifa wa Umar (Allah amridhie), Zainab alifariki dunia huko Madina. Baada ya kuoshwa na kuvikwa sanda, Waislamu –wakiongozwa na Amiril-muominina Umar - walimswalia, na kuzikwa katika viwanja vya Baqii.

Walioingia kaburini kwa ajili ya kumzika walikuwa ni Usama bin Zaid, Muhammad bin Abdullah bin Jahsh na Abdullah bin abi Ahmad bin Jahsh. Allah amridhie Zainab, mama wa Waislamu, na amrehemu, amin.



AFYA YAKO

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Utafiti: Hakuna uvutaji tumbaku 'kidogo usio na madhara'



Kwa muda mrefu watu wengi wameamini kwamba "sigara moja moja tu" haiwezi kuleta madhara makubwa kiafya. Utafiti mpya ulioripotiwa na tovuti ya Healthline unavunja kabisa imani hii. Watafiti wamebaini kuwa hata kuvuta sigara chache sana kwa siku, kama mbili pekee, kunaongeza hatari ya magonjwa ya moyo na vifo kwa kiwango cha kutisha. Matokeo haya ni ukumbusho kwamba hakuna kiwango salama cha uvutaji sigara. Uvutaji "wa mara chache" bado ni sumu

Kwa mujibu wa utafiti huo, watu wanaovuta sigara kati ya mbili hadi tano kwa siku wanaongeza hatari ya shambulio la moyo kwa takribani asilimia 57, na kufa kwa asilimia 60 ikilinganishwa na wale ambao hawajawahi kuvuta sigara. Hii inaonyesha wazi kuwa hata "sigara za starehe tu" au "za wikiendi" siyo salama.

Watafiti walichambua taarifa za zaidi ya watu 300,000 kutoka tafiti 22 za muda mrefu, baadhi yao wakifuatiliwa hadi miaka 20. Katika kipindi hicho, kulikuwa na vifo 125,000 na matukio 54,000 ya magonjwa ya moyo na mishipa kama vile mshtuko wa moyo, kiharusi na shambulio la moyo. Takwimu hizi zinatoa uzito wa kisayansi unaoacha nafasi ndogo ya kukanusha.

Cha kutia moyo ni kwamba hatari hupungua kadiri muda unavyopita baada ya kuacha sigara, hasa ndani ya miaka 10 ya mwanzo. Hata hivyo, Healthline inaonyesha kuwa hata baada ya miongo mitatu, aliyewahi kuvuta sigara bado anaweza kubaki na hatari kubwa zaidi kuliko yule ambaye hakuwahi kuanza kabisa. Hii ndiyo maana ujumbe mkuu wa watafiti ni huu: ni bora kuacha mapema, na ni bora zaidi kutokuanza kabisa.

## Jinsi sigara inavyoharibu moyo hata kwa kiwango kidogo

Wataalamu walioulizwa na Healthline wanasema hatari ya sigara siyo "sawa sawa" kadiri sigara zinavyoongezeka. Sigara za mwanzo ndizo zinazofanya madhara makubwa zaidi kwenye mfumo wa moyo na mishipa na kuongeza uwezekano wa damu kuganda, mishipa kuziba na hatimaye mshtuko wa moyo au kiharusi. Haya hutokea hata kwa sigara moja hadi mbili kwa sik.,

Kwa maneno mengine, mwili haupimi "idadi ndogo" ya moshi kama salama. Mara tu sumu zinapoingia, zinaanzisha mfululizo wa madhara, hata kama sigara hazikutumiwa kwa wingi.

## Uharibifu hauishii kwenye moyo pekee

Healthline inakumbusha pia kwamba kemikali hatari kwenye moshi wa tumbaku huathiri karibu kila kiungo cha mwili. Zaidi ya watu milioni 16 nchini Marekani wana magonjwa yanayohusiana moja kwa moja na sigara. Uvutaji huongeza hatari ya zaidi ya aina 10 za saratani, husababisha magonjwa ya mapafu kama C pumu, huongeza uwezekano wa kupata kisukari aina ya pili, na hata magonjwa ya macho.

Takwimu za CDC zinazotajwa na Healthline zinaonyesha kuwa uvutaji sigara na moshi wa sigara kwa wasiovuta husababisha zaidi ya vifo 480,000 kila mwaka Marekani, sawa na karibu moja kati ya vifo vitano. Ujumbe wa madaktari ni wazi: sigara ni adui wa mwili mzima, siyo wa mapafu peke yake.

## Kuacha sigara: safari ngumu lakini inawezekana

Licha ya hatari zote hizi, kuacha sigara si rahisi. Healthline inaeleza kuwa takribani theluthi mbili ya wavutaji wangependa kuacha, na zaidi ya nusu tayari wameshawahi kujaribu. Siri ya mafanikio iko kwenye kuchanganya mbinu kadhaa.

Wataalamu wa afya wanashauri mtu aanze kwa kutambua sababu zinazomfanya avute, aweke tarehe maalumu ya kuacha, na ajitengenezee mpango wa kubadilisha tabia hiyo kwa shughuli nyingine zenye afya. Msaada wa kitabibu unaweza kupunguza hamu kali ya kuvuta. Ushauri nasaha na vikundi vya msaada husaidia kukabiliana na upande wa kisaikolojia, hasa wakati wa msongo wa mawazo na vishawishi.

Daktari Kevin Shah, akizungumza na Healthline, anakumbusha kuwa kurudi kuvuta baada ya kujaribu kuacha si kushindwa, bali ni sehemu ya safari. Wale wanaotumia mchanganyiko wa mbinu, na kupata msaada kutoka kwa madaktari, familia na marafiki, wana nafasi kubwa zaidi ya kuacha kabisa.

Kilicho wazi ni kwamba hakuna uvutaji kidogo usio na madhara". Sigara mbili kwa siku tu zinatosha kuutupa moyo kwenye hatari kubwa. Uamuzi wa busara, iwe kwa kijana anayeanza "kujaribu" au mtu mzima anayevuta "mara chache", ni mmoja tu: acha sasa, huku bado una nafasi ya kulinda miaka yako ijayo.


Sikiliza Radio
Imaan FM
Dar es Salaam 104.5fm
Arusha 90.8fm
Mwanza 106.5fm
Mbeya 90.3fm
Tabora 101.6fm
Ruvuma 94.2fm
Mtwara 90.9fm
Kigoma 92.5fm
/radioimaanfm
MOROGORO
96.3 fm
MSAMVU
twiga
Elimu Bila Mipaka



# Kipimo cha uongozi ni kuwasamehe unaowaongoza

Imepokewa hadith kutoka kwa Ibn Abbas (Allah amridhie yeye na baba yake) kwamba, Uyainah bin Hisn bin Hudhayfah alifika katika mji wa Madina na kufikia kwa mpwa wake aitwae Al–Hurr bin Qays. Al–Hurr alikuwa mmoja wa watu ambao Amir wa Waumin, Umar bin Khattwab (Allah amridhie) aliwafanya kuwa karibu yake, na alikuwa miongoni mwa wasomaji wa Qur'an (amehifadhi na kuielewa vizuri Qur'an), pia alikuwa katika watu wanaopendelea kukaa kwenye vikao vya Umar akimshauri mambo mbalimbali.

Uyainah alimwambia mpwa wake: "Ewe mpwa wangu, je una nafasi mbele ya huyu kiongozi? Nifanyie mpango nipate ruhusa ili niingie kwake." Al–Hurr akasema: "Nitakuombea ruhusa." Ibn Abbas (Allah amridhie) akasema: "Al–Hurr alishamwombea ruhusa Uyainah, Umar akamruhusu aingie ndani kuonana naye."

Uyainah alipoingia ndani alisema: "Sikiliza ewe mwana wa Al–Khattwab! Wallahi hautupi mali kwa utoshelevu, wala hautuhukumu kwa uadilifu!" Umar alikasirika sana kiasi cha kutaka kumdhuru Uyainah.

Al–Hurr akamwambia Umar: "Ewe Amirul Muuminin, hakika Allah Mtukufu alimwambia Mtume wake (rehema na amani zimshukie): 'Shikamana na usamehevu, amrisha mema, na jiepushe na majahili (wajinga).'" [Qur'an, 7:199]. Na huyu (Uyainah) ni miongoni mwa watu wajinga. Ibn Abbas akasema: "Naapa kwa Allah! Umar hakuvuka mipaka ya aya hii baada ya kusomewa, na alikuwa mtu aliyesimama madhubuti katika Kitabu cha Allah. ***[Bukhari]***."

## Mafundisho ya tukio hili

Uislamu unatukataza kumnasihi au kumkosoa kiongozi hadharani, kwani jambo hilo humfedhehesha na kumvunjia heshima. Hutokea baadhi ya nyakati watu wakakiuka mafundisho haya kutokana na tabia zao au mazingira waliyokulia, ambayo huwafanya kuwa mbali na mafundisho ya Uislamu.

Iwapo hilo litatokea, ni vyema kiongozi akawa mvumilivu na mwenye huruma zaidi badala ya kutoa adhabu. Uyainah alimtamkia Umar maneno makali na ya kuudhi, lakini Umar alipokumbushwa aya ya Qur'an inayomtaka asamehe alirudi nyuma na kuacha adhabu aliyokusudia kuitoa.

Hatua hii inatufundisha kuwa, daima kiongozi anatakiwa kuwa na subira, uvumilivu na kutojihusisha na kisasi binafsi.

## Mamlaka yamewekwa kwa ajili ya kuhudumia watu

Umar (Allah amridhie) alikuwa na uwezo wa kumwadhibu Uyainah, lakini hakutumia mamlaka yake vibaya. Uislamu unasisitiza kuwa, kiongozi hakuwekwa ili ailinde nafsi yake au kulipiza kisasi, bali yeye ni mtumishi wa watu.

Mtume (rehema na amani zimshukie) alikuwa hamlipizii mtu kisasi hata kama mtu huyo amemuudhi au kumfanyia uadui. Yeye alikuwa mkali na mwenye kulipiza kisasi pale tu mtu anapovuka mipaka ya Allah Mtukufu, na aghalabu alikuwa akiwashika mkono wale waliomkosea na kuwaongoza katika njia iliyonyooka.

Raia siyo malaika; wanaweza kukosea kwa maneno au vitendo. Kwa kutambua hilo, Uislamu unawataka viongozi wawe wasamehevu, na wanapowakemea watu basi wafanye hivyo kwa hekima na wasiwaharibie maisha yao kwa makosa madogo madogo.

Umar (Allah amridhie) alipokumbushwa ujumbe wa Qur'an: "Shikamana na msamaha, amrisha mema, na jiepushe na wajinga," moyo wake ulitulia. Kiongozi yeyote ni lazima ashikamane na Kitabu cha Allah (Qur'an) katika kuwaongoza watu, na siyo kufuata hisia au mitazamo ya watu.

Na linapotokea jambo baya au linalomchukiza ahakikishe havuki mipaka ya Allah Ta'ala katika kulishughulikia. Kuna wakati kiongozi hupotezwa au kutelezeshwa na washauri wake kutokana na maslahi binafsi wanayoyapata. Kwa hiyo, kiongozi anatakiwa awe makini sana hata kwa watu anaowaamini, kwani binadamu wana tabia ya kukengeuka na kusukumwa na matamanio. Kiongozi anatakiwa kuzungukwa na watu wenye elimu, hekima, busara na wachamungu. Hawa ndiyo wanapaswa kuwa washauri bora kwake, kwa sababu wana 'macho' ya ziada katika kumshauri.

Tukimtazama Mtume (rehema na amani zimshukie) katika nyanja zote za maisha yake; kuanzia cheo cha Utume, kiongozi wa jamii, baba wa familia, mume, na rafiki kwa wale waliomzunguka, tunaona alikuwa mwepesi sana wa kusamehe.

Mtume aliwasamehe Makureish baada ya kuukomboa mji wa Makka licha ya kupanga njama za kumuua, aliwasamehe watu wa Twaif ambao walimpiga mawe na kumfukuza katika mji wao, pia aliwasamehe na kuwavumilia wanafiki katika mji wa Madina licha ya madhila waliyokuwa wakimfanyia.

Huu ni mfano mwema wa kuigwa kwa kiongozi mwenye haja ya kujifunza na kufanya lililo bora zaidi kwa watu wake.

## Tuwaheshimu viongozi

Kumheshimu kiongozi ni miongoni mwa misingi imara ya taifa bora lililojengwa kwa kuzingatia maadili na tabia njema. Watu wanaomvunjia heshima kiongozi wao hawatambui nafasi ya maadili na tabia njema katika kujenga utu na taifa lao.

Iwapo kiongozi atapoteza hadhi yake, ni wazi taifa zima litafedheheka na kudharaulika, kwa sababu kiongozi wao ameshapoteza hadhi na heshima yake. Uislamu unakataza kuwadharau na kuwavunjia heshima viongozi, na hata ikibidi kuwakosoa basi isiwe hadharani.

Hakuna binadamu mkamilifu hapa duniani, hivyo tunapoona kiongozi amekosea tutumie busara na njia bora za kutatua matatizo badala ya kujiingiza kwenye mambo yenye madhara na mwisho mbaya.

## Mtume ﷺ amesema:

"Muislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wamesalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake, na Muhajir (mhamaji wa kweli) ni yule anayeacha kile alichokataza Mwenyezi Mungu."

Bukhari





JUNAYNAT ALLY DAMA

# Je, watoto wa chekechea wafanyishwe mtihani?

Kila mara mjadala kuhusu mitihani shuleni unapozuka, jamii hugawanyika. Lakini swali linapohamia kwa watoto wa chekechea—wenye umri wa miaka minne au mitano—mjadala huu hauwi tu wa kitaaluma bali wa kiroho, kibinadamu na kimaadili. Je, ni sahihi kuwapeleka watoto wadogo kabisa katika ulimwengu wa mitihani? Je, wanaandaliwa au wanakandamizwa? Na, kama mitihani haina budi kuwepo, inapaswa kufanywa vipi ili isiwe mzigo kwao?

Ripoti kutoka nchi mbalimbali zimejaribu kuanzisha majaribio kwa wanaoanza shule kama kipimo cha kuangalia maendeleo yao baadaye. Serikali hutetea hatua hii kwa madai kuwa inarahisisha kupima uwezo wa shule na mapungufu ya mtoto. Lakini swali linalowatia wasiwasi wazazi na walimu wengi ni: Je, mtoto wa miaka minne ana mahitaji ya kipimo hiki? Je, anahitaji alama, uchambuzi au hatia katika miaka ambayo bado anajifunza kutambua hisia zake mwenyewe?

Wataalamu wengi wa malezi wanaonya kwamba miaka ya chekechea ni kipindi cha dhahabu cha ukuaji wa ubongo. Ndani ya kipindi hiki, mtoto anahitaji michezo ya kujenga misuli, lugha, fikra, ushirikiano, utu na uwezo wa kujihisi salama.

Mitihani ya mapema ina hatari ya kuingiza watoto katika "ulimwengu wa maumivu ya kihisia" kabla hawajakua vya kutosha kuelewa maana ya kushindwa. Kwa mtoto mdogo, kushindwa si suala la "hakuna alama," bali "mimi si mzuri." Hii ndiyo hatari ya msingi.

Waalimu wengi ambao wamejaribu aina hizi za mitihani wameeleza jinsi watoto wanavyotatizika kufuata maagizo ya mtihani, kuzingatia, au kuelewa dhana ya "jibu sahihi." Mfano wa mwanafunzi wa chekechea aliyetakiwa kubaini maana ya neno "sokoni" unaonyesha dhahiri tatizo hili.

Kwa mtoto, "market" inaweza kuwa sehemu ya kwenda na mama na kucheka. Kwa hivyo, anaposikia sentensi kama "Ninacheza mpira kwenye sokoni," katika fikra yake hakuna tatizo—kwa sababu ubunifu wake haujawahi kuwekewa mipaka. Kwa hiyo, kumhukumu kuwa "ameshindwa" ni kutokuelewa kabisa dunia ya mtoto.

Pia, mitihani ya mapema huepusha mtoto na masomo muhimu ya maisha—life skills—ambayo ndiyo msingi wa mafanikio yake ya baadaye. Badala ya kuwauliza maswali ya chaguo la herufi, watoto wanahitaji kupewa nafasi ya kushirikiana, kujadiliana, kupanga vitu, kuuliza maswali, kushindwa bila kuumia, na kuendelea kujaribu. Haya ndiyo maisha halisi, na ndiyo msingi wa elimu ya kweli.



Kwa upande mwingine, hoja ya kwamba mitihani inaweza kusaidia kubaini changamoto za ukuaji si ya kupuuzwa. Walimu na wataalam wa saikolojia wanaweza kutumia tathmini laini (observational assessments) kubaini areas zinazohitaji msaada bila kumweka mtoto kwenye shinikizo. Hata hivyo, tathmini hizi haziwezi kuwa mitihani ya karatasi, alama, au ushindani.

## Kama lazima tahadhari ichukuliwe

Kama mfumo wa elimu utaamua kwamba mitihani ya chekechea haiwezi kuepukika, basi angalau mambo mawili makubwa yazingatiwe ili kuepusha madhara:

Kwanza, kuepuka majibu magumu yanayohitaji jibu moja tu sahihi. Mitihani yenye majibu yaliyofungwa "kwa lazima" huzuia ubunifu wa mtoto na kumfundisha kufikiri kwa kufuata mashine, si kwa kufikiri kwa umakinifu. Mitihani inayotumia uchoraji, kutaja vitu, kusimulia hadithi, au michezo midogo ndiyo inayolingana zaidi na umri wao.

Pili, kuepuka kuwapanga watoto wa kwanza hadi wa mwisho, jambo ambalo ni sumu kwa hisia zao. Kupangwa chini humfanya mtoto aamue kuwa yeye ni duni. Wengine hutoka darasani wakiwa na huzuni, wakijihisi dhaifu au wasiostahili. Haya ni majeraha ya kihisia ambayo yanaweza kudumu kwa miaka.

Badala ya mitihani kuwa hukumu, inaweza kuwa tukio la maendeleo, mazungumzo na mwalimu, tathmini ya kimtazamo, au ushahidi wa hatua ya ukuaji. Matokeo yasiwekwe kwenye mbao, yasilinganishwe na ya wengine, na yasitumike kumwambia mtoto "wewe si mzuri."

Kwa mtazamo mpana, mjadala huu si tu kuhusu mitihani. Ni mjadala kuhusu utu wa watoto, namna tunavyoelewa ukuaji, na aina ya jamii tunayojenga. Tukilazimisha mitihani mapema, tunawasukuma watoto kwenye ulimwengu wa watu wazima kabla hawajakomaa. Tukichelewa, tunawapa muda wa kujenga msingi imara wa fikra, hisia na uhusiano.

Kwa hiyo, swali halisi si "Watoto waanze mitihani lini," bali "Tunataka watoto wetu wawe watu wa aina gani?" Na jibu hilo linahitaji hekima, si haraka; utafiti, si shinikizo; na zaidi ya yote, moyo wa kutanguliza utu wa mtoto kabla ya mfumo wa alama.





UKHTI FATIMA SS

# Kwa nini watu hunyanyasa wenzao?

**Unyanyasaji, hasa wa kimwili, kisaikolojia na kupitia mitandao, umegeuka kuwa jambo la kawaida katika maeneo mbalimbali ya kijamii ikiwemo taasisi za elimu, mahali pa kazi, ndani ya familia na kadhalika. Wengi wetu tunaujua uchungu wa kudharauliwa, kuitwa majina mabaya au kutengwa makusudi. Lakini kichwani mwa mnyanyasaji nini hutokea? Kuelewa saikolojia ya unyanyasaji hutusaidia kujilinda, kulinda watoto zetu, vijana na hata watu wazima.**

## Mizani ya nguvu isiyo sawa

Kwanza, wanasaikolojia wanaeleza kwamba unyanyasaji ni tendo la mtu mwenye nguvu au hadhi kubwa kutumia nafasi hiyo kumdhuru aliye dhaifu kwa kurudia-rudia. Kiini chake ni hoja ya nguvu na udhibiti – yaani mtu anajisikia juu pale tu anapomfanya mwingine ajisikie mdogo.

Ni kwa msingi huo ndio maana unyanyasaji huonekana sana pale penye mizani ya nguvu isiyo sawa: mwanafunzi mbabe dhidi ya asiye na marafiki, bosi dhidi ya mfanyakazi, kundi kubwa dhidi ya mtu mmoja.

## Watoto wanapoiga kunyakua nguvu

Watoto na vijana hujifunza kunyakua nguvu kwa kuiga. Nadharia ya ujifunzaji kijamii inaonyesha kuwa tukiona tabia fulani ikizawadiwa na kusifiwa, basib tunaikariri na kutamani tuwe hivyo. Filamu, muziki na michezo ya video inapomtukuza "mkali" anayewadhalilisha wengine na kushangiliwa, ujumbe usiosemwa ni kwamba ukali unalipa.

Vile vile, mtoto anayekua kwenye nyumba yenye familia yenye matusi, ubabe, adhabu za kupiga na ugomvi usiokoma wa wazazi, basi huanza kuona vurugu kama njia ya kawaida ya kutatua matatizo na kuiga.

## Kutojiamini

Saikolojia pia inaonyesha sura ya ndani ya mnyanyasaji. Wengine wanaonekana wajasiri, lakini ndani wamejaa hofu na kutokujiamini. Hivyo basi, ili wasionekane wanyonge, wanatangulia kuwashambulia wengine.

Mwingine anapojiona dhaifu kwenye masomo, umbo au hali ya kiuchumi, anaweza kutafuta mtu "mrahisi" wa kumkandamiza ili ajione bora. Kwao, kudhalilisha ni mkakati wa kuficha majeraha yao wenyewe.

## Mazoea

Sababu nyingine ni mazoea ya mafanikio ya haraka. Mtu akigundua kuwa akipaza sauti, kutisha au kusambaza tetesi anapata anachotaka kwa haraka – cheo, uongozi wa darasa au umaarufu – ubongo hujenga uhusiano: ukali = ushindi. Bila kupewa mbinu mbadala za mawasiliano, tabia hii huota mizizi na hubadilika kuwa mtindo wa maisha.

Sio wote wanaonyanyasa kwa kuonekana wazi. Wapo wanaotumia unyanyasaji wa mahusiano: kumtenga mtu kimakundi, kumzushia maneno au kumfanya aonekane kichekesho. Huu ni unyanyasaji wa ndani kwa ndani, lakini maumivu yake ya kisaikolojia ni makali kama kupigwa.

Kwa ujumla, m,saada wa kitaalamu unaweza kuwasaidia wanyanyasaji kujifunza kudhibiti hasira, kutatua migogoro bila vurugu na kutafuta heshima bila kumuumiza mwingine.

## Unyonge wa waathirika na ukimya wa mashuhuda

Tafiti zinaonyesha kuwa wanaolengwa mara nyingi huonekana wanyenyekevu kupita kiasi, wenye wasiwasi au tofauti fulani – umbile, ulemavu, rangi, dini, mwelekeo wa kijinsia. Hata hivyo, kosa si lao. Wanapodhalilishwa mara kwa mara, huanza kujiangalia kwa macho ya mnyanyasaji na kujihisi duni. Hali hii inaweza kuleta mfadhaiko, wasiwasi na hata mawazo ya kujiua. Ushauri nasaha, vikundi vya msaada, na wazazi wanaosikiliza kwa makini vinaweza kusaidia sana kurejesha hali ya kujiamini ya wanaonyanyaswa.

Tafiti za "bystander effect" (mashuhuda) zinaonyesha kwamba kadiri watu wanavyokuwa wengi, ndivyo kila mmoja anavyojisemea "Atakuwapo mwingine wa kuingilia." Ukimya wao unampa mnyanyasaji nguvu zaidi na kumwonyesha mwathiriwa kuwa yupo peke yake. Lakini jambo la kutia moyo ni kwamba mtu mmoja tu akisimama na kusema, "Hii si sawa," mizani ya nguvu hubadilika.

Teknolojia ya kidijitali yaongeza ujasiri

Katika enzi ya kidijitali, unyanyasaji huu umehamia pia mtandaoni – ujumbe wa kejeli, akaunti za uongo, picha zinazochafua hadhi. Kutokana na kificho cha skrini, mnyanyasaji huhisi hatafikiwi na hatapatikana, na hivyo ujasiri wa ukatili huongezeka.

## Hatua moja kuelekea utatuzi

Kuelewa saikolojia ya unyanyasaji ni hatua moja kuelekea utatuzio. Kufahamu huko hutukumbusha kwamba tabia hii ni matokeo ya majeraha, mifumo ya nguvu na mafunzo mabaya. Suluhisho la kudumu linahitaji zaidi ya adhabu: linahitaji kulea huruma, kuwafundisha watoto mbinu salama za kutatua migogoro, kuwapa waathiriwa msaada wa kisaikolojia na kuwaelimisha watazamaji kwamba ukimya wao ni sehemu ya tatizo.



# Sanaa ya mazungumzo: Kutoafiki wazo bila kumvunjia mtu heshima

Katika maisha ya kila siku, tofauti za maoni haziwezi kuepukika. Tunaweza kubishana nyumbani, kazini, shuleni, kwenye makundi ya WhatsApp au mitandaoni.
Tatizo halipo kwenye kutofautiana, bali namna tunavyowasilisha hayo mawazo. Inawezekana kabisa kutokubaliana na mtu bila kumkashifu, kumuumiza au kumdhalilisha. Hii ndiyo sanaa ya mazungumzo yenye staha—kilele cha ukomavu wa kiakili na kihisia ambacho kila mtu anaweza kujifunza.

## Sikiliza kwanza kabla ya kujibu

Hatua ya kwanza ya kutokubaliana kwa heshima ni kusikiliza kwa makini. Mpe mwenzako nafasi ya kueleza msimamo wake bila kumkatiza, bila kumrushia hoja za kujihami, na bila kutafuta maneno ya kumjibu kabla hajamaliza. Ukisikiliza kwa moyo wazi, unampa ujumbe kwamba unamheshimu hata kama hamtamaliza mkikubaliana.

Maswali ya kutafuta kuelewa, kama "Unaweza kufafanua zaidi?" au "Umefikiaje hitimisho hilo?", yanaunda mazingira ya ushirikiano badala ya ugomvi. Hata ukipingana naye baadaye, atajua kwamba ulitoka mahali pa heshima.

## Tenganisha mtu na wazo

Tatizo kubwa la mijadala mingi ni kuchukulia wazo kama utu wa mtu. Badala ya kusema "Wewe huelewi chochote", unaweza kusema "Mimi naona hili kwa namna tofauti".

Hoja inaposhambuliwa badala ya mtu, unajenga daraja la maelewano. Lugha ya kuhukumu kama "Sikuzote", "Kila mara" au "Wewe huwa..." hufunga milango ya mazungumzo na kumfanya mwingine ajihami. Kutoafikiana hakumaanishi kumshambulia mtu binafsi—ni kutofautiana juu ya fikra

## Tumia lugha laini

Kauli zinazoanza na "Wewe" husikika kama shambulio na hujenga ukuta wa hisia. Badala ya kusema "Wewe umekosea", jaribu "Mimi nahisi kama kuna taarifa zaidi tungehitaji". Hapa unaonyesha mtazamo wako bila kumwekea hatia mwingine.

Pia, maneno kama "labda", "pengine", "huenda" au "kwa mtazamo wangu" hupooza ukali wa hoja na kuifanya ipokelewe kwa utulivu. Kwa njia hii, unaweza kutoa pingamizi zito bila kuliumiza upande wa pili.

## Tafuta msingi wa pamoja kupunguza mvutano

Kabla hujapingana, jaribu kuona ni wapi mnafanana. Hata kama mnatofautiana sana, mara nyingi kuna nukta ndogo mnayokubaliana. Unaweza kusema "Nakubaliana nawe kuwa suala hili ni muhimu; tofauti yetu ni njia ya kulitatua."

Mbinu hii inageuza mazungumzo kutoka mapambano kwenda kuwa ushirikiano. Kukiri pale mwingine alipo sahihi hakupunguzi nguvu ya hoja yako bali kunaongeza heshima kwa unayeongea naye na kudhihirisha busara yako.

## Uliza maswali yanayofungua mazungumzo

Maswali ni nyenzo bora ya kuondoa hisia za kupambana. Badala ya kusema "Hilo si kweli", unaweza kuuliza maswali kama: "Ni kitu gani kimekufanya uamini hivyo?" au "Kuna mfano mwingine ambao umeona?"

Katika muktadha huu, maswali yanapunguza hitilafu za mawasiliano na mara nyingi hufichua mizizi ya hoja kuliko mabishano ya moja kwa moja. Mazungumzo yanapogeuka kuwa uchunguzi wa pamoja, hata kutokubaliana kuna ladha ya kujifunza.

## Dhibiti hisia: ukimya wa dakika moja si kushindwa

Wakati mwingine, kujadili tofauti za mawazo kunaweza kuamsha hasira. Ishara za mwili—kumpandisha na kumshusha kwa macho, kuinua mabega kwa dharau, au kucheka kwa dhihaka—huchoma zaidi kuliko maneno.

Ukihisi mori unakupanda, pumua kwa kina na zungumza polepole. Inawezekana pia kuomba muda kwa kusema "Naona nimeanza kukasirika, hebu tuchukue dakika kidogo." Ukomavu wa mjadala si uwezo wa kushambulia, bali ujasiri wa kujituliza.

## Kubali uwezekano wa kukosea

Mazungumzo ya staha hutengeneza nafasi ya kubadilishana mitazamo, na hii inawezekana tu ukikubali kuwa unaweza kukosea.

Kauli kama "inawezekana sijaelewa vizuri, lakini mtazamo wangu ni..." zinaonyesha unyonge mzuri unaowezesha mwingine kufungua moyo wake. Wakati mwingine, kukubali kuwa fikra zako zinaweza kurekebishwa kunaleta nguvu kuliko kusisitiza kwamba wewe ndio uko sahihi.

## Tafuta namna ya kusonga mbele

Lengo la kutokubaliana si kushinda hoja bali kuelewana. Unaweza kupendekeza mwelekeo wa pamoja kama "Tujaribu njia hii kwanza kisha tutathmini", au hata kukubaliana kuwa hamtakubaliana lakini bado mtabaki marafiki, wenzake au ndugu wanaoheshimiana. Kutokubaliana si mwisho wa mahusiano; ukosefu wa adabu ndio huua kila kitu.

Nimalize kwa kusema kuwa kutoafikiana si kuonyeshana ubabe wala kudhalilishana. Ni sehemu ya ukuaji wa kiakili na kijamii.